



**SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR**

**OFISI YA RAIS NA MWENYEKITI WA BARAZA  
LA MAPINDUZI**

**HOTUBA YA WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS NA  
MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI**

**MHESHIMIWA ISSA HAJI USSI GAVU  
KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI  
YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA**

**2019/2020**

**MEI, 2019**

## **YALIYOMO**

YALIYOMO .....	ii
ORODHA YA VIAMBATISHO .....	iii
VIFUPISHO VYA MANENO .....	iv
1. UTANGULIZI .....	1
2. UTEKELEZAJI WA PROGRAMU ZA OFISI YA RAIS NA MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI KWA KIPINDI CHA JULAI – MACHI 2018/2019 .....	6
2.1 UPATIKANAJI WA FEDHA ZA UTEKELEZAJI WA PROGRAMU ZA OFISI .....	7
2.2 MAFANIKIO YALIYOPATIKANA KATIKA UTEKELEZAJI WA PROGRAMU ZA OFISI YA RAIS NA MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI KWA KIPINDI CHA JULAI – MACHI 2018/2019 .....	7
3. MWELEKEO WA BAJETI YA OFISI YA RAIS NA MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020 .....	53
4. PROGRAMU KUBWA NA NDOGO NA MAKISIO YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020 .....	56
5. MAOMBI YA FEDHA KWA KAZI ZILIZOPANGWA KUTEKELEZWA KATIKA MWAKA WA FEDHA 2019/2020 .....	66
5.1 MATUMIZI YA KAWAIDA NA MIRADI YA MAENDELEO .....	66
5.2 MAOMBI YA FEDHA 2019/2020 .....	67
6. HITIMISHO .....	67

## **ORODHA YA VIAMBATISHO**

Kiambatisho Nam. 1: Mapitio ya Upatikanaji wa Fedha kwa Kazi za Kawaida 2018/2019	71
Kiambatisho Nam. 2: Orodha ya Shehia zilizooneshwa Sinema	76
Kiambatisho Nam. 3: Orodha ya Vipindi Vilivyorushwa Hewani na Idara ya Mawasiliano na Habari Ikulu – Zanzibar Kupitia Kituo cha ZBC Radio (A)	77
Kiambatisho Nam. 4: Idadi ya Wafanyakazi Waliopatiwa Mafunzo	82
Kiambatisho Nam. 5: Idadi ya Watumishi Waliokwenda likizo	85
Kiambatisho Nam. 6: Idadi ya Wafanyakazi waliofanyiwa upekuzi na Taasisi walizotoka	86
Kiambatisho Nam. 7: Orodha ya Taasisi Zilizofanyiwa Ukaguzi wa Kiusalama	90
Kiambatisho Nam. 8: Idadi ya Watumishi Waliopewa Mafunzo ya Udhhibiti wa Siri na Utunzaji wa Nyaraka za Serikali	91
Kiambatisho Nam. 9: Orodha ya Nyaraka za Sera na Sheria Zilizojadiliwa na Baraza la Mapinduzi	92
Kiambatisho Nam. 10 : Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Bajeti 2019/2020	94
Kiambatisho Nam. 11 : Orodha ya Wageni Waliofika Ikulu na Kuonana na Mheshimiwa Dk. Ali Mohamed Shein – Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Kuanzia Mwezi wa Julai, 2018 Hadi Mwezi wa Aprili, 2019	99

## VIFUPISHO VYA MANENO

ACP	African Carribean Pacific Group of States (Mashirikiano ya Nchi za Afrika, Carribean na Pasifiki)
APRM	African Peer Review Mechanism (Mpango wa Nchi za Afrika Kujitathmini Kiuchumi, Kidemokrasia na Utawala Bora)
CCM	Chama Cha Mapinduzi
COMESA	Common Market for Eastern and Southern Africa (Soko la Pamoja la Nchi za Mashariki na Kusini mwa Afrika)
COSTECH	Tanzania Commission for Science and Technology (Tume ya Sayansi na Teknolojia Tanzania)
EAC	East African Community (Jumuiya ya Afrika Mashariki)
EPA	Economic Partnership Agreements (Mkatoba wa Ubia wa Kiuchumi)
GSO	Government Security Office (Ofisi ya Usalama wa Serikali)
IORA	Indian Ocean Rim Association (Jumuiya ya Nchi zilizopakana na Bahari ya Hindi)
IPA	Institute of Public Administration (Chuo cha Utawala wa Umma Zanzibar)
KIST	Karume Institute of Science and Technology (Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Karume)
MKUZA	Mpango wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Zanzibar
MOU	Memorandum Of Understanding (Mkatoba wa Makubaliano)
ORMBLM	Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi

SADC	Southern Africa Development Community (Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika)
SMZ	Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar
SUZA	State University of Zanzibar (Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar)
TEHAMA	Teknolojioa ya Habari na Mawasilino
TZS	Tanzania Shillings (Shilingi ya Tanzania)
UAE	United Arab Emirates (Umoja wa Falme za Kiarabu)
ZACADIA	Zanzibar Canada Diaspora Association (Jumuiya ya Wanadiaspora wa Zanzibar wanaoishi Canada)
ZBC	Zanzibar Broadcasting Company (Shirika la Utangazaji Zanzibar)
ZIPA	Zanzibar Investment Promotion Authority (Mamlaka ya Vitega Uchumi Zanzibar)
ZPDC	Zanzibar Petroleum Development Corporation (Kampuni ya Maendeleo ya Mafuta Zanzibar)
ZU	Zanzibar University (Chuo Kikuu cha Zanzibar)



## 1. UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako tukufu, likae kama Kamati kwa ajili ya kupokea, kujadili, kuzingatia na hatimae kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa mwaka wa fedha 2019/2020.
2. **Mheshimiwa Spika**, kila sifa njema anastahiki Mwenyezi Mungu Mtukufu mwingi wa rehema na utukufu. Tunamshukuru Yeye kwa kutujaalia kukutana hapa tukiwa wazima na wenye afya njema. Vile vile namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nguvu na uwezo wa kuwasilisha Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 kwenye Baraza lako hili tukufu. Namuomba Mwenyezi Mungu aendelee kutuzidishia siha njema, amani na utulivu katika nchi yetu.
3. **Mheshimiwa Spika**, kwa heshima naomba kuchukua fursa hii adhimu kumpongeza Mheshimiwa Dk. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa uongozi wake uliojaa hekima na busara. Juhudi, umakini na umahiri wake umeiwezesha Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuitekeleza Ilani ya Uchaguzi Mkuu ya CCM ya mwaka 2015-2020 kwa zaidi ya asilimia 90. Utekelezaji huo unakwenda

sambamba na malengo ya Dira ya Maendeleo ya 2020 pamoja na Mpango wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini Zanzibar Awamu ya Tatu (MKUZA III). Namuomba Mwenyezi Mungu amzidishie afya njema yeye na familia yake, ili aendelee kuwatumikia wananchi wa Zanzibar na kuwaletea maendeleo ya haraka zaidi.

4. **Mheshimiwa Spika**, nampongeza kwa dhati Mheshimiwa Balazi Seif Ali Iddi, Makamu wa Pili wa Rais Zanzibar kwa namna anavyomsaidia na kumshauri Mheshimiwa Dk. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi pamoja na Ofisi yetu kiujumla katika kutekeleza majukumu yatu. Pamoja na kuwa anakabiliwa na majukumu mengi ya Kitaifa, pia amekuwa mstari wa mbele katika kuwatumikia wananchi wa Jimbo la Kitope. Ni imani yetu kuwa wananchi wa Jimbo hilo wataendelea kumpatia ushirikiano, ili aendelee kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi.
5. **Mheshimiwa Spika**, pongezi maalum nazileta kwako Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid, Spika wa Baraza la Wawakilishi kwa namna unavyoliongoza na kulisimamia Baraza lako Tukufu. Kadhalika, nampongeza Naibu Spika Mheshimiwa Mgeni Hassan Juma pamoja na Mheshimiwa Mwanaasha Khamis Juma na Mheshimiwa Shehe Hamad Mattar Wenyeviti wa Baraza hili kwa namna wanavyokusaidia katika kazi zako za Baraza.



6. **Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya kipekee nampongeza Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa, Mheshimiwa Panya Ali Abdalla kwanza kwa kuchaguliwa kwake kuwa Mwenyekiti wa Kamati hii na pili kwa uwezo wake wa hali ya juu katika kusimamia dhamana aliyokabidhiwa. Vile vile, nampongeza Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Ali Suleiman Ali (Shihata) pamoja na Waheshimiwa wajumbe wote wa Kamati hii. Ni imani yangu tutaendelea kushirikiana nao katika kutekeleza ipasavyo majukumu yetu tuliyokabidhiwa.
7. **Mheshimiwa Spika**, kwa dhati kabisa natoa pongezi kwa Waheshimiwa Wenyeviti wa Kamati ya Bajeti Mheshimiwa Mohammed Said Mohammed (Dimwa) na Kamati ya Kudhibiti na Kuchuguza Hesabu za Serikali Mheshimiwa Miraji Khamis Mussa (Kwaza) na Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati hizi kwa ushirikiano mzuri wa kikazi na ORMBLM. Mwisho naomba kumalizia pongezi zangu kwa Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi kwa michango, pongezi, ushauri na maelekezo mazuri ambayo kwa namna moja au nyengine yamekuwa yakijenga na kutusaidia katika kutekeleza na kutimiza majukumu yetu ipasavyo.

8. **Mheshimiwa Spika**, nitakuwa sijatenda haki bila ya kuwapongeza wananchi wa Zanzibar kwa imani na upendo wao wa dhati katika kumuunga mkono Mheshimiwa Dk. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa juhudi zake za kuiletea maendeleo Zanzibar. Wito wangu kwa wananchi wote wa Zanzibar waendeleo kumuunga mkono na kushirikiana nae kikamilifu kwa maslahi ya kila mmoja wetu.
  
9. **Mheshimiwa Spika**, tarehe 30 Aprili, 2019 Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imepata msiba kufuatia kifo cha Ndugu Juma Ali Juma, aliyekuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Biashara na Viwanda kilichotokea katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, Dar es Salaam. Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi imepokea kwa mshtuko na huzuni taarifa ya kifo hicho. Marehemu Juma Ali Juma atakumbukwa kwa juhudi, uadilifu na mchango wake mkubwa katika utekelezaji wa majukumu yake. ORMBLM inaungana na wanafamilia katika kuomboleza msiba huu katika kipindi hiki kigumu. Namuomba Mwenyezi Mungu ailaze roho ya Marehemu mahali pema Peponi. Amin.
  
10. **Mheshimiwa Spika**, msimu wa mvua tayari umenza katika visiwa vyetu. Katika miongo ya hivi karibuni, tumeshuhudia mvua kuwa kubwa zikinyesha katika maeneo yetu ambazo husababisha athari mbali mbali kwa wananchi.

Aidha, wataalamu wa hali ya hewa wametabiri kuwa katika msimu huu wa mvua kutakuwa na mvua kubwa ambazo zitakuwa za wastani au juu ya wastani kwa baadhi ya maeneo. Hivyo, naomba kutoa wito kwa wananchi wote kuchukua tahadhari zinazostahiki, ili kujiepusha na athari zinazoweza kujitokeza. Kwa upande mwingine, nawaomba wananchi wazitumie vizuri mvua hizi kwa kupanda miti na mazao mengine ya chakula.

11. **Mheshimiwa Spika**, huu ni mwezi mtukufu wa Ramadhani, Waislamu wa hapa Zanzibar wanajumuika na waislamu wenzao kote duniani kufunga mwezi huu mtukufu. Mwezi huu huambatana na ibada na kufanyiana mambo mema kwa jamii yetu. Namuomba Mwenyezi Mungu atujaalie funga njema na baraka tele, ili atukubalie funga zetu na atulipe malipo mema.
12. **Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo ya utangulizi, sasa naomba uniruhusu niwasilishie Utekelezaji wa Programu za Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kipindi cha Julai – Machi, 2018/2019.

**2. UTEKELEZAJI WA PROGRAMU ZA OFISI YA RAIS NA MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI KWA KIPINDI CHA JULAI – MACHI 2018/2019**

**13. Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa mwaka wa fedha 2018/2019 imetekeleza Programu Kuu tano na Programu Ndogo 11 chini ya Mafungu mawili ambayo ni Fungu A01 na A02. Programu Kuu hizo ni:-

- i. Programu ya Kusimamia Huduma na Kuratibu Shughuli za Mheshimiwa Rais na Kuimarisha Mawasiliano Ikulu,
- ii. Programu ya Kuratibu Ushirikiano wa Kikanda, Mashirika ya Kimataifa na Wazanzibari Wanaoishi Nje ya Nchi,
- iii. Programu ya Utumishi na Uendeshaji wa Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi,
- iv. Programu ya Usimamizi wa Majukumu ya Kikatiba na Kisheria ya Baraza la Mapinduzi na Kamati ya Makatibu Wakuu, na
- v. Programu ya Utumishi na Uendeshaji wa Ofisi ya Baraza la Mapinduzi.

**14. Mheshimiwa Spika,** Utekelezaji wa Programu hizi, umezingatia Mipango Mkuu ya Kitaifa ikiwemo Ilani ya Uchaguzi Mkuu ya CCM ya mwaka 2015 – 2020, Mpango wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Zanzibar (MKUZA) pamoja na Mpango Mkakati wa Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

## **2.1 UPATIKANAJI WA FEDHA ZA UTEKELEZAJI WA PROGRAMU**

- 15. Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2018/2019, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi iliidhinishiwa jumla ya TZS. milioni 10,433.7 kwa mafungu yake mawili. Fungu A01 lilitengewa jumla ya TZS. milioni 8,472.1. Kati ya hizo TZS. milioni 1,000.0 kwa ajili ya mradi wa maendeleo na TZS. Milioni 7,472.1 kwa ajili ya kazi za kawaida. Fungu A02 lilitengewa jumla ya TZS. milioni 1,961.6 kwa kazi za kawaida. Hadi kufikia mwezi Machi, 2019 Fungu A01 lilingiziwa jumla ya TZS. milioni 5,936.5 sawa na asilimia 79 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na TZS. milioni 999.9 sawa na asilimia 99.9 kwa ajili ya mradi wa maendeleo. Aidha, fungu A02 lilingiziwa TZS. milioni 1,388.7 sawa na asilimia 92 (Kiambatisho Nam. 1) kinatoa ufafanuzi.

## **2.2 MAFANIKIO YALIYOPATIKANA KATIKA UTEKELEZAJI PROGRAMU ZA OFISI YA RAIS NA MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI KWA KIPINDI CHA JULAI – MACHI 2018/2019**

- 16. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Julai – Machi 2018/2019, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ilitekeleza Programu zake kwa ufanisi na kupata mafanikio yafuatayo:-

## **Programu ya Kusimamia Huduma na Kuratibu Shughuli za Mheshimiwa Rais na Kuimarisha Mawasiliano Ikulu**

- 17. Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2018/2019, Programu hii iliidhinishiwa TZS. milioni 4,998.7 kwa matumizi ya kawaida na maendeleo. Hadi kufikia mwezi Machi, 2019 iliingiziwa jumla ya TZS. milioni 4,668.1 sawa na asilimia 93 kwa kazi za kawaida na TZS. milioni 999.9 sawa na asilimia 99.9 kwa kazi za maendeleo.
  
- 18. Mheshimiwa Spika**, shughuli mbali mbali katika Programu hii zimeratibiwa na kutekelezwa kwa ufanisi. Wananchi wameweza kufikiwa katika maeneo yao kutokana na ziara ambazo Mheshimiwa Rais amezifanya katika Wilaya zote za Unguja na Pemba. Vile vile, mawasiliano baina ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na wananchi yamezidi kuimarika kutokana na utoaji wa haraka wa taarifa kwenye vyombo vya habari na mitandao ya kijamii.
  
- 19. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2018/2019, Mheshimiwa Dk. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi alifanya ziara mbili nje ya nchi kwa lengo la kuimarisha uhusiano, kuongeza fursa za kiuchumi na kijamii pamoja na kuitangaza Zanzibar.

20. **Mheshimiwa Spika**, ziara ya mwanzo ya Mheshimiwa Rais ilifanyika nchini Indonesia tarehe 31 Julai hadi 6 Agosti, 2018. Katika ziara hio, Mheshimiwa Rais alikutana mwenyeji wake Mheshimiwa Muhammad Jusuf Kalla, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Indonesia. Katika mazungumzo yao, viongozi hao walikubaliana kuimarisha uhusiano baina ya Zanzibar na Indonesia pamoja na kuendeleza Biashara, Uwekezaji na Kilimo hasa katika zao la mpunga, mwani na minazi.
21. **Mheshimiwa Spika**, masuala mengine waliyokubaliana ni kuendeleza ushirikiano katika Sekta ya Uvuvi, Uwekezaji, Viwanda Vidogo Vidogo na vya Kati, Elimu, Afya, Utalii (ukiwemo usafiri wa anga), Utafiti, Utamaduni na uimarishaji wa Miundombinu ya Bandari ya Mafuta na Gesi Asilia. Mheshimiwa Makamu wa Rais aliahidi kwamba Indonesia itaisaidia Zanzibar vifaa na nyenzo za uvuvi pamoja na kuiwezesha kusafirisha samaki na viumbe vyengine vya baharini.
22. **Mheshimiwa Spika**, akiwa katika ziara ya Indonesia, Mheshimiwa Rais, vile vile, alikutana na Uongozi na wanachama wa Jumuiya ya Wafanyabiashara na Wenyewiwanda ya Indonesia (KADIN). Aliwaelezea kuhusu hali ya amani na utulivu iliyopo Zanzibar na kuwahamasisha waje wawekeze Zanzibar ambapo watafaidika na soko la ndani, soko la nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki pamoja na Jumuiya ya Maendeleo ya

Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC). Katika ziara hio, Zanzibar ilizitangaza fursa za uwekezaji zilizopo nchini ambazo ziliwavutia sana wawekezaji wa Indonesia.

- 23. Mheshimiwa Spika**, vile vile, Mheshimiwa Rais na ujumbe wake walifanya mazungumzo na Uongozi wa Kampuni ya Mafuta na Gesi ya Indonesia iitwayo Pertamina. Viongozi wa Kampuni hio wameonesha nia ya kuja kuwekeza Zanzibar na mawasiliano yanaendelezwa. Kadhalika, Mheshimiwa Rais na ujumbe wake ulifanya mazungumzo na Uongozi wa Benki ya Exim ya Indonesia.
- 24. Mheshimiwa Spika**, katika mazungumzo hayo, ilikubalika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iunde timu maalum itakayokwenda Indonesia kuendeleza mazungumzo na Benki hio. Vile vile, ujumbe wa Benki ya Exim ulitembelea Zanzibar kuona fursa zilizopo kwa lengo la kufanikisha uwekezaji. Hatua hizo zimeshafanyika ambapo Benki ya Exim ya Indonesia imo katika hatua za mwisho za kufanya makubaliano na Benki ya Afrika, ili itoe mkopo nafuu wa ujenzi wa Bandari ya Gesi Asilia ya Mangapwani.
- 25. Mheshimiwa Spika**, wakati akiwa nchini Indonesia, Mheshimiwa Rais na ujumbe wake walikutana na Uongozi wa Mamlaka ya Kusimamia Uwekezaji ya Indonesia. Ujumbe wa Zanzibar ulielezwa juu ya namna ambavyo Indonesia imefanikiwa katika



kuimarisha mitaji binafsi na kuongeza ajira kwa vijana. Pande hizo mbili zilikubaliana kubadilishana taarifa juu ya fursa za uwekezaji na kutembeleana. Uongozi wa Mamlaka ya Uwekezaji ya Indonesia umeahidi kuzitangaza fursa za uwekezaji za Zanzibar nchini Indonesia. Ujumbe maalum wa Serikali ya Indonesia umezuru Zanzibar na kukutana na Viongozi na Watendaji wa SMZ.

- 26. Mheshimiwa Spika,** katika uimarishaji wa Sekta ya uvuvi na kilimo cha mwani, ujumbe wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ulikutana na kufanya mazungumzo na viongozi wa Indonesia wanaosimamia Sekta ya uvuvi, kilimo na mwani. Baada ya mazungumzo baina ya pande hizo mbili zilikubaliana ufanywe utafiti utakaowezesha kujua wastani wa wingi wa samaki katika bahari ya Zanzibar.
- 27. Mheshimiwa Spika,** viongozi hao, vile vile walikubaliana kubadilishana uzoefu wa kufanya doria na udhibiti wa uvuvi haramu, kutoa mafunzo kwa wavuvi wadogo wadogo, kuanzisha ushirikiano baina ya Kampuni ya Uvuvi ya Indonesia na Kampuni ya Uvuvi ya Zanzibar (ZAFICO) na kusaini Hati ya Maelewano (MoU) baina pande mbili hizo.
- 28. Mheshimiwa Spika,** kadhalika, Mheshimiwa Rais na ujumbe wake walitembelea Kampuni ya kusarifu Samaki na viumbe wengine wa baharini iitwayo

Perikanan Indonesia, iliyopo Jakarta. Uongozi wa Kampuni hio umekubali kuja Zanzibar kuisaidia Kampuni ya ZAFICO katika kuimarisha shughuli za uvuvi. Hati ya Maelewano (MoU) katika sekta ya uvuvi imewasilishwa kwa Mwanasheria Mkuu kwa kupatiwa muongozo wa kisheria.

**29. Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa kilimo na mazao ya biashara, Viongozi wa Taasisi za Kilimo za Indonesia na Ujumbe wa Zanzibar, walikubaliana kuwa na ushirikiano katika utafiti na elimu kwa wakulima. Vile vile, Indonesia imeombwa ianzishe kiwanda cha uwanga wa unga wa muhogo kwa ajili ya kutengenezea mifuko isiyochafua mazingira. Kadhalika, Mheshimiwa Rais na ujumbe wake walikutana na uongozi wa Kampuni ya Samani Virgin Coconut Oil Industry ambapo ilikubalika mawasiliano baina ya pande mbili hizo yaendelezwe. Hivi sasa Serikali imo katika hatua za mwisho za kukamilisha kutia saina Hati ya Maelewano na Indonesia.

**30. Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa uimarishaji wa Sekta ya Kilimo na Mazao ya Biashara, Mheshimiwa Rais na ujumbe wake walikutana na kufanya mazungumzo na Meya wa Jimbo la Galantano, Profesa Nelson Pomalingo ambae ni Mtaalamu wa Kilimo na Minazi. Katika mazungumzo yao, walikubaliana kushirikiana katika kudhibiti maradhi ya minazi na kufanya utafiti wa zao hilo. Ujumbe wa Zanzibar, vile vile

ulitembelea kiwanda cha kusarifu zao la mwani kiitwacho PT Agar Swallow.

- 31. Mheshimiwa Spika,** Uongozi wa kiwanda hicho umekubali kushirikiana na Zanzibar katika kuliendeleza zao la mwani. Kadhalika, ujumbe wa Zanzibar ulitembelea kiwanda cha kusindika majani ya mimea, ikiwemo majani makavu ya mikarafuu kwa ajili ya kutoa mafuta ya viungo. Uongozi wa kiwanda hicho ulikubali kuja Zanzibar kwa ajili ya kuwekeza na kushirikiana na wakulima katika utengenezaji wa mafuta ya viungo. Uongozi wa kampuni hio umeshafika Zanzibar mara kadhaa ambapo hatua za uingiaji wa makubaliano ya ubia na ZSTC zinaendelea vizuri na uzalishaji wa majaribio utanza mwaka 2019.
- 32. Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa utalii, Mheshimiwa Dk. Ali Mohamed Shein alikutana na kufanya mazungumzo na Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni ya Maendeleo ya Utalii (ITDC) wa Indonesia pamoja na kutembelea Chuo cha Utalii kilichopo Bali. Chuo hicho kinatoa Shahada na Stashahada katika nyanja za utalii na ukarimu. Makubaliano yaliyofikiwa ni kwamba Chuo Kikuu hicho kiko tayari kutoa mafunzo kwa Wazanzibari katika nyanja ya utalii, kufanya ziara za kubadilishana utalaamu na kuandaa mkakati wa pamoja utakaowafanya watalii watumie muda zaidi wanapotembelea Zanzibar.

- 33. Mheshimiwa Spika,** aidha, Viongozi hao wawili walikubaliana kuandaa programu ya mafunzo ya utalii ya pamoja baina ya Zanzibar na Indonesia. Kadhalika, kuanzisha ushirikiano baina ya Chuo cha Utalii cha Bali na Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA). Kampuni ya Utalii ya Indonesia imekubali kuitembelea Zanzibar kuja kuona uwezekano wa kujenga hoteli. Hatua za ukamilishaji wa Hati ya Maelewano baina ya Zanzibar na Indonesia katika Sekta ya Utalii zimeshachukuliwa na matayarisho yanaendelea.
- 34. Mheshimiwa Spika,** kwa jumla, ziara rasmi ya Mheshimiwa Dk. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi nchini Indonesia ilikuwa ni ya mafanikio na imezidi kufungua milango ya ushirikiano baina ya nchi hizi mbili. Viongozi wa sekta mbali mbali yakiwemo mashirika ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na viongozi wa Taasisi za umma na makampuni ya Indonesia, wameanza utaratibu wa kutembeleana, kubadilishana mawazo na kutekeleza mipango ya kuimarisha sekta za huduma, fedha, miundombinu, kilimo, biashara na viwanda.
- 35. Mheshimiwa Spika,** Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dk. Ali Mohamed Shein, alifanya ziara nyengine nchini Kenya kuanzia tarehe 25 hadi 28 Novemba, 2018. Katika ziara hio, Mheshimiwa Rais

alimuwakilisha Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Mkutano wa Kimataifa wa Uchumi Endelevu wa Bahari, uliofanyika Nairobi.

- 36. Mheshimiwa Spika,** katika Mkutano huo, Mheshimiwa Rais alitoa tamko la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tamko hilo, lilitilia mkazo kwa Mataifa Duniani kuitumia vizuri rasilimali ya bahari, mito na maziwa pamoja na rasilimali nyenginezo zilizomo humo katika kuleta mageuzi ya kiuchumi. Kadhalika, tamko hilo, limezingatia mabadiliko ya tabia nchi yanayotoa changamoto zinazosababisha upungufu wa wingi wa samaki katika bahari, mito na maziwa pamoja na ongezeko la bidhaa za plastiki baharini na maeneo mengine ya maji.
- 37. Mheshimiwa Spika,** vile vile, katika tamko hilo, imeelezwa kwamba juhudi za pamoja zinahitajika Kitaifa na Kimataifa katika kukabiliana na changamoto zilizopo. Aidha, tamko limesisitiza haja ya kuendeleza ajenda na mipango ya kuimarisha uchumi wa bahari maarufu kwa jina la “Blue Economy”.
- 38. Mheshimiwa Spika,** akiwa nchini Kenya, Mheshimiwa Rais alifanya mazungumzo na Mheshimiwa Uhuru Muigai Jomo Kenyatta, Rais wa Jamhuri ya Kenya ambapo walikubaliana kuendeleza uhusiano wa kindugu na kihistoria

wa nchi hizi mbili. Kadhalika, viongozi hao walikubaliana kuwa wataalamu wa nchi hizi kutembeleana na kubadilishana utaalumu katika Sekta ya Uvuvi wa Bahari Kuu na udhibiti wa uvuvi haramu.

- 39. Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa uimarishaji wa Sekta ya Utalii, viongozi hao wamekubaliana paanzishwe safari za ndege za Shirika la Ndege la Kenya, za moja kwa moja, baina ya Mombasa na Zanzibar. Vile vile, viongozi hao wamekubaliana kuwa safari za meli ya MV Mapinduzi II ziimarishwe na ziendelezwe baina ya Zanzibar na Mombasa.
- 40. Mheshimiwa Spika,** alipokuwa ziarani nchini Kenya, Dk. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi alifanya mazungumzo na viongozi wa Jumuiya ya Kaunti za Ukanda wa Pwani ya Kenya. Kaunti hizo ni Mombasa, Kwale, Kilifi, Tana River, Lamu na Taita Taveta. Mazungumzo yao yalihusu kuimarisha misingi ya ujirani mwema hasa kwa kuzingatia asili ya watu wa mwambao.
- 41. Mheshimiwa Spika,** masuala mengine yaliyozungumzwa ni kuanzishwa kwa ziara za Magavana wa Kaunti za Pwani ya Kenya na Wakuu wa Mikoa na Viongozi wa ngazi mbali mbali kutoka Zanzibar. Vile vile, walikubaliana kuwa ziara hizo za viongozi zilenge katika kuimarisha sekta ya utalii kwa kuvishirikisha vyo vikiu. Kadhalika,

walizungumzia haja ya kuwaondolea usumbufu wavuvi wadogo wadogo wa maeneo yetu pamoja na kuliimarisha zao la mwani.

42. **Mheshimiwa Spika**, viongozi wengine ambao Mheshimiwa Rais alikutana nao ni Rais wa Sychelles; Mheshimiwa Danny Faure. Katika mazungumzo yao, walikubaliana kuimarisha ushirikiano baina ya nchi hizi mbili. Vile vile, katika kukuza biashara na utalii walikubaliana kuanzisha safari za ndege za moja kwa moja kati ya Zanzibar na Sychelles kupitia Shirika la Ndege la Sychelles (Ushelisheli).
43. **Mheshimiwa Spika**, ziara ya Mheshimiwa Rais nchini Kenya, pia, ilimuwezesha kukutana na Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia masuala ya mazingira (UNEP), Dk. Joyce Msuya. Miongoni mwa mambo yaliyozungumzwa na kuafikiwa ni Shirika hilo kuendelea kufanya kazi kwa karibu na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika mambo yanayohusu mazingira. Kadhalika, Shirika la UNEP liliahidi kusaidia kufundisha wataalamu wa mazingira wanaohitajika katika Sekta ya Mafuta na Gesi na masuala yote muhimu kwa uchumi na maendeleo ya Zanzibar.
44. **Mheshimiwa Spika**, katika shughuli zake za kikazi za ndani ya nchi, kwa mara nyengine Mheshimiwa Rais alikuwa mgeni rasmi katika hafla ya ufunguzi

wa Kongamano la Diaspora lililofanyika katika Viwanja vya Tibirinzi Pemba tarehe 18 na 19 Agosti, 2018. Katika hotuba yake, aliendelea kuwakumbusha na kuwataka Wanadiaspora kuendeleza uzalendo na mapenzi ya nchi yao kwa kuhakikisha kwamba wanashiriki kikamilifu katika utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya Zanzibar na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa jumla, ikiwemo kuwekeza nyumbani.

45. **Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa ziara za ndani, katika mwaka wa fedha 2018/2019, Mheshimiwa Dk. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi alifanya ziara katika Wilaya 11 za Unguja na Pemba. Katika ziara hizo, alizindua na kuweka mawe ya msingi katika miradi mbali mbali ya maendeleo pamoja na kuzungumza na viongozi na wananchi.
46. **Mheshimiwa Spika**, katika Wilaya ya Mjini, Mheshimiwa Rais aliweka jiwe la msingi la Mradi wa ujenzi wa tangi la maji safi na salama liliopo Kilimani (Mnara wa Mbao) na Saateni. Miradi hio kwa pamoja ina thamani ya USD\$ milioni 24 zikiwemo USD\$ milioni 3 zilizotolewa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Kukamilika kwa miradi hio, kutapunguza kwa kiasi kikubwa tatizo la upungufu wa huduma za maji safi na salama katika shehia 27 za Mkoa wa Mjini Magharibi.



47. **Mheshimiwa Spika**, katika Wilaya ya Magharibi 'A', Mheshimiwa Rais aliweka jiwe la msingi katika kituo cha afya cha Kianga ambacho kimejengwa kwa udhamini wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF). Hivi sasa, kituo hicho, kiko katika hatua za mwisho za kukamilika, ili kiweze kutumika na kuwaondolea usumbufu wananchi wa kufuata huduma za Afya katika maeneo ya mbali.
48. **Mheshimiwa Spika**, vile vile, akiwa katika Wilaya hio, alitembelea shughuli za wajasiriamali wanaojishughulisha na uanikaji wa dagaa katika eneo la Kihinani. Katika eneo hilo, aliweka jiwe la msingi la jengo la wajasiriamali hao. Mheshimiwa Rais, aliwahakikishia wajasiriamali hao, kwamba Serikali iko pamoja nao katika juhudi zao za kujajiri wenyewe.
49. **Mheshimiwa Spika**, katika Wilaya ya Magharibi 'B', Mheshimiwa Rais aliweka jiwe la msingi katika Skuli ya msingi ya Kwarara inayojengwa kwa msaada wa majirani wema NGO ya Jamhuri ya Korea Kusini. Kukamilika kwa ujenzi wa skuli hio, kutaondosha tatizo la msongamano wa wanafunzi katika skuli za karibu na eneo hilo. Vile vile, katika Wilaya hio, Mheshimiwa Rais aliweka jiwe la msingi la kituo cha afya cha Magirisi katika Jimbo la Kijitoupele. Baada ya kukamilika, Kituo hicho kilichoanza kujengwa kwa nguvu za wananchi, kitatumiwa na wananchi wa eneo hilo na maeneo ya jirani kwa ajili ya kupata huduma za msingi za afya.

- 50. Mheshimiwa Spika,** katika ziara yake ya Wilaya ya Kaskazini 'B', Mheshimiwa Rais alitembelea maeneo yanayochimbwa mchanga ya Pangatupu, Chechele na Kiombamvua. Katika maelezo yake, Mheshimiwa Rais alieleza kusikitishwa kwake na hali ya kumalizika mchanga kwenye machimbo hayo na uharibifu mkubwa wa mazingira iliyotokana na uchimbaji wa mchanga usiozingatia sheria. Aliagiza iundwe Kamati Maalum ya kusimamia utekelezaji wa maelekezo ya shughuli za uchimbaji wa mchanga.
- 51. Mheshimiwa Spika,** katika Wilaya ya Kaskazini A, Mheshimiwa Rais aliweka jiwe la msingi la Skuli ya Sekondari ya Kijini inayojengwa kwa ushirikiano wa wananchi na wawekezaji & Beyond Mnemba Island Logde na African Foundation. Katika hotuba yake, aliwapongeza wawekezaji kwa michango yao katika kuimarisha huduma za jamii. Vile vile, aliwataka wananchi kuendeleza juhudi za kilimo cha mwani kwa vile Serikali imeandaa mipango madhubuti ya kuliimarisha zao hilo.
- 52. Mheshimiwa Spika,** katika Wilaya ya Kati, Mheshimiwa Rais aliweka jiwe la msingi katika Skuli ya msingi ya Ng'ambwa inayojengwa kwa nguvu za wananchi. Akizungumza na wananchi, Mheshimiwa Rais aliitaka Wizara ya Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati isimamie matengenezo ya tangi la maji la Unguja Ukuu, ili huduma za maji safi na salama ziweze kuwafikia wananchi wa Uzi na Ng'ambwa.

- 53. Mheshimiwa Spika,** kadhalika, Mheshimiwa Rais aliiagiza Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji kusimamia ujenzi wa barabara kutoka Unguja Ukuu Kaepwani hadi Kisiwa cha Uzi pamoja na kufikiria mpango ya ujenzi wa daraja litakalounganisha Kisiwa hicho na sehemu ya Unguja Ukuu.
- 54. Mheshimiwa Spika,** katika Wilaya ya Kusini Unguja, Mheshimiwa Rais aliwataka Viongozi na wananchi wa Wilaya hio, kuacha kujihusisha na migogoro ya ardhi na kwamba ile iliyopo ishughulikiwe. Vile vile, alihimiza hali ya usalama wa raia na mali zao iimarishwe pamoja na vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia vidhibitwiwe ipasavyo.
- 55. Mheshimiwa Spika,** katika Wilaya ya Mkoani, Mheshimiwa Rais aliweka jiwe la msingi la barabara ya Mkanyageni – Kangani. Ujenzi wa barabara hio, ni muhimu katika kufanikisha usafiri wa wananchi na usafirishaji wa mazao mbali mbali ikiwemo zao la karafuu linalopatikana kwa wingi katika maeneo hayo. Aidha, Mheshimiwa Rais alifungua Skuli ya Sekondari ya Michenzani, Mkoani ikiwa ni miongoni mwa jitihada za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar za kuimarisha elimu ya Sekondari.
- 56. Mheshimiwa Spika,** katika Wilaya ya Chake Chake, Mheshimiwa Rais alifungua barabara ya Kuyuni – Ngomeni. Vile vile, Mheshimiwa Rais alifungua Kituo cha afya cha kisasa cha Ngomeni

ikiwa ni Kituo cha kwanza katika eneo hilo. Ujenzi wa Kituo hicho, ni utekelezaji wa ahadi alioitwa Mheshimiwa Rais ya kujenga Kituo cha afya katika eneo hilo.

57. **Mheshimiwa Spika**, katika Wilaya ya Wete, Mheshimiwa Rais, aliweka jiwe la msingi la Skuli ya msingi ya Bopwe na aliifungua Skuli ya Sekondari ya Mchangamdogo. Katika hotuba yake, alisisitiza juu ya haja ya kuongeza idadi ya madarasa, ili kupunguza msongamano wa wanafunzi madarasani. Miradi hio yote ya sekta ya elimu, inakwenda sambamba na dhamira ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kuimarisha mazingira bora ya elimu.
58. **Mheshimiwa Spika**, kwenye Wilaya ya Micheweni, Mheshimiwa Rais alikagua maeneo ya yanayochimbwa mchanga ya Finya Selem na Shumba Viamboni, ili kuona hali halisi ya maeneo hayo ya kuchimbwa mchanga kwa upande wa Pemba. Katika nasaha zake, Mheshimiwa Rais alisisitiza kuwa utaratibu wa uchimbaji wa mchanga uzingatiwe na kusimamiwa vizuri na taasisi zinazohusika.
59. **Mheshimiwa Spika**, vile vile, Mheshimiwa Rais alisisitiza kuchukua hatua za haraka za kuyaimarisha maeneo yanayochimbwa mchanga kwa upandaji wa miti na utunzaji wa mazingira. Kadhalika, Mheshimiwa Rais alilizindua jengo la

mikutano la Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni. Alisistiza kwamba jengo hilo litunzwe na litumike vizuri kwa utoaji wa huduma za wananchi na shughuli mbali mbali za kijamii zilizokusudiwa.

- 60. Mheshimiwa Spika**, kwa jumla, Mheshimiwa Rais kwenye hotuba zake za majumuisho alizozitoa katika kila Wilaya, aliwahimiza wananchi waendeleo kushirikiana na Serikali katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kadhalika, alisisitiza haja ya kuimairisha umoja, amani na mshikamano na kuongeza kasi ya kuipatia ufumbuzi migogoro ya ardhi na kuizuia mipya isitokee.
- 61. Mheshimiwa Spika**, vile vile, Mheshimiwa Rais aliwataka Waheshimiwa Wabunge, Wawakilishi na viongozi mbali mbali kuwa karibu na wananchi kwa kuwapa taarifa juu ya utekelezaji wa mipango ya maendeleo. Kadhalika, aliwahimiza viongozi hao kujitathmini juu ya utekelezaji wa ahadi walizotoa wakati wa kampeni na kuzingatia kwamba muda wa Uchaguzi Mkuu unakaribia na wananchi watawapima kwa utekelezaji wa ahadi walizozitoa.
- 62. Mheshimiwa Spika**, Mheshimiwa Rais kwa wakati tofuati, alikuwa Mgeni Rasmi katika mahafali ya Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar, (SUZA), Chuo Kikuu cha Zanzibar (ZU) na Chuo Kikuu cha Abdulrahman Al-Sumait kiliopo Chukwani. Katika hotuba zake kwenye mahafali hizo, alisisitiza umuhimu wa

Vyuo vikuu kutoa elimu inayokwenda sambamba na mipango ya maendeleo ya nchi, mahitaji ya soko la ajira pamoja na kutoa wahitimu wenye uwezo wa kujiajiri wenyewe. Kadhalika, alihimiza umuhimu wa Vyuo Vikuu kuongeza juhudi katika kufanya tafiti ikiwa ni nyenzo muhimu ya kutatua changamoto zinazoikabili jamii.

- 63. Mheshimiwa Spika,** vile vile, Mheshimiwa Rais aliwaalika Ikulu wanafunzi waliofanya vizuri katika mitihani ya Taifa ya kidato cha nne na cha sita iliyopita. Aliwaandalia wanafunzi hao hafla maalum ya kuwapongeza. Katika hotuba yake, Mheshimiwa Rais aliwahimiza wanafunzi hao kuongeza bidii katika masomo yao, ili waendeleo kufanya vizuri zaidi katika ngazi za masomo zinazofuata. Vile vile, aliahidi kuongeza fursa za udhamini za Serikali kwa wanafunzi wa kidato cha sita wanaofanya vizuri, kutoka nafasi 15 hadi 30, hatua ambayo tayari imeshachukuliwa.
- 64. Mheshimiwa Spika,** tarehe 28 Agosti 2018, Mheshimiwa Rais, alizindua programu ya pamoja baina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inayoendeshwa na Mashirika ya Umoja wa Mataifa. Katika uzinduzi huo, alitoa shukrani kwa Umoja wa Mataifa kwa kuiunga mkono Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika utekelezaji wa mipango ya maendeleo. Aidha, Mheshimiwa Rais alieleza kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inathamini sana mashirikiano na

misaada inayoipata kutoka Umoja wa Mataifa katika kuendeleza sekta ya elimu, afya, utawala bora na mapambano dhidi ya udhalilishaji. Vile vile, Mheshimiwa Rais aliahidi kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itaimarisha na itaendeleza ushirikiano mzuri na Umoja wa Mataifa.

**65. Mheshimiwa Spika,** tarehe 11 Oktoba, 2018, Mheshimiwa Rais alifungua maonesho ya siku ya Chakula Duniani yaliyofanyika katika kijiji cha Chamanangwe Pemba na kuwasihi vijana wazitumie vilivyo fursa za ajira zilizopo katika sekta ya kilimo, ufugaji na uvuvi katika kukabiliana na changamoto za uhaba wa ajira Serikalini. Alieleza kwamba Serikali imeandaa mazingira mazuri ya kuwasaidia vijana kwa kuwapatia mafunzo na mitaji ya kuendeshea shughuli za kilimo kupitia Mfuko wa Uwezesaji.

**66. Mheshimiwa Spika,** katika suala la kuimarisha utalii, Mheshimiwa Rais alishiriki katika maonesho ya utalii yaliyofanyika tarehe 17 Oktoba, 2018, Mtoni, katika Hoteli Verde. Maonesho hayo yamesaidia kuitangaza Zanzibar duniani kote kwa kiasi kikubwa. Wawekezaji walioshiriki katika maonesho hayo, walielezwa juu ya uwekezaji unaohitajika hapa Zanzibar na kuyaelewa mazingira halisi ya visiwa vya Unguja na Pemba. Mheshimiwa Rais alisema kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itahakikisha kuwa sekta ya utalii inainufaisha jamii yote kwa jumla ikiwa

ni miongoni mwa utekelezaji wa mfumo wa utalii kwa wote.

- 67. Mheshimiwa Spika,** tarehe 23 Oktoba, 2018 Mheshimiwa Dk. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi pamoja na Sheikh Saud bin Saqr Al Qasimi; Mtawala wa Ras Al Khaimah walishuhudia utiaji wa saina Mkataba wa Mgawanyo wa Uzalishaji wa Mafuta na Gesi Asilia, Ikulu Zanzibar.
- 68. Mheshimiwa Spika,** katika hafla hio, Mheshimiwa Rais alisema kuwa suala la utafutaji wa mafuta na gesi asilia ni jambo linalohusu maendeleo ya Zanzibar na kamwe halitakiwi kuleta mfarakano katika jamii yetu, badala yake linatakiwa lituunganishe. Aliwataka wananchi wajiepushe na watu wachache ambao wameamua kulitumia jambo hili kuwa ajenda ya kuwagawa watu jambo ambalo ni kinyume na malengo ya Serikali.
- 69. Mheshimiwa Spika,** vile vile, Mheshimiwa Rais alieleza kwamba, malengo ya Serikali ni kuhakikisha kuwa faida zitakazopatikana kutokana na rasilimali ya mafuta na gesi asilia zinachangia katika ukuaji wa uchumi na kuwanufaisha wananchi wote. Mheshimiwa Rais aliendelea kusema kuwa uzalishaji wa mafuta na gesi utapelekea kuimarika kwa uchumi wetu na kunawiri kwa hali ya nchi yetu na maisha ya watu wake. Kadhalika, alisisitiza kwamba litakuwa ni jukumu la Serikali ya



Mapinduzi ya Zanzibar kuwapa taarifa wananchi zinazohusu masuala yote ya mafuta na gesi asilia hapa Zanzibar. Taarifa hizo, zitatolewa na Waziri anaeshughulikia mambo ya nishati au wasaidizi wake na si mtu mwengine yoyote.

- 70. Mheshimiwa Spika,** katika risala ya kuukaribisha mwaka mpya wa 2019, Mheshimiwa Rais aliwahimiza Viongozi wajitathmini katika utekelezaji wa ahadi walizozitoa wakati wa uchaguzi mkuu na watekeleze majukumu yao wakitambua kwamba muda wa uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020 unakaribia. Mheshimiwa Rais aliwaelezea Viongozi na wananchi kwamba yamepatikana maendeleo makubwa kupitia utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi Mkuu ya CCM ya mwaka 2015-2020. Mheshimiwa Rais alihimiza wananchi washirikiane katika shughuli mbali mbali za kiuchumi na maendeleo ya jamii na kuhimiza mshikamano.
- 71. Mheshimiwa Spika,** katika maadhimisho ya Sherehe za Miaka 55 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar, Mheshimiwa Rais aliweka jiwe la msingi la jengo la Wizara ya Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati pamoja na Mamlaka ya Udhubiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA). Kadhalika, Mheshimiwa Rais alivifungua vituo vya uokozi vya KMKM Kibweni na Mkoani Pemba, ambavyo vitafanya kazi ya uokoaji wa maisha ya wananchi pale maafa yanapotokezea.

- 72. Mheshimiwa Spika,** katika sherehe hizo, Mheshimiwa Rais, vile vile, aliufungua Uwanja wa Michezo wa Mao tse Tung uliopo Kikwajuni ambao utaongeza idadi ya viwanja vikubwa vya michezo vinavyoweza kutumika hata kwa michezo ya kimataifa. Kadhalika, Mheshimiwa Rais aliifungua barabara ya Kijito Upele – Fuoni hatua ambayo itaimarisha huduma za usafiri kwa wananchi na wakaazi wanaotumia barabara hio. Vile vile, Mheshimiwa Rais alilifungua jengo la Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali liliopo Maruhubi. Katika hotuba yake, alisema kwamba kuwepo kwa mitambo ya kisasa ya kupimia vinasaba (DNA) ndani ya maabara hio, kutaondoa changamoto iliyokuwepo ya kupata huduma hizo hapa Zanzibar.
- 73. Mheshimiwa Spika,** katika kilele cha Sherehe za Maadhimisho ya Miaka 55 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar, yaliyofanyika katika Uwanja wa Michezo wa Gombani, Pemba tarehe 12 Januari, 2019; Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi alijumuika na wananchi na Viongozi mbali mbali ambapo yeye alikuwa ndie Mgeni rasmi kama ilivyo desturi.
- 74. Mheshimiwa Spika,** katika hotuba aliyoitoa kwenye sherehe hizo, Mheshimiwa Rais alielezea mafanikio yaliyopatikana katika kuendeleza uchumi wa Zanzibar na katika sekta za Elimu, Afya, Kilimo, Maji, Mawasiliano, Nishati, Mazingira,

Michezo na nyinginezo. Aliwahimiza wananchi wafanye kazi kwa bidii na alieleza kwamba amani, utulivu, mshikamano ndio jawabu pekee za kutatua changamoto zinazotukabili. Kadhalika, alisisitiza juu ya umuhimu wa kuitunza amani ya nchi yetu kwa faida ya kila mmoja wetu.

- 75. Mheshimiwa Spika**, tarehe 26 Februari, 2019, Mheshimiwa Rais aliufungua Mkutano wa Bunge la Afrika Mashariki. Katika nasaha zake aliwasisitiza Wabunge wa Bunge hilo, kuongeza kasi ya mapambano dhidi ya rushwa, ikizingatiwa kuwa vitendo vya rushwa vinazorotesha uchumi na maendeleo. Vile vile, Mheshimiwa Rais alihimiza juu ya umuhimu wa Bunge hilo katika kuitangaza lugha ya Kiswahili katika ngazi ya Kimataifa.
- 76. Mheshimiwa Spika**, Kadhalika, Mheshimiwa Rais alitoa shukurani kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa kuichagua Zanzibar kuwa Makao Makuu ya Kamisheni ya Kiswahili ya Afrika Mashariki. Vile vile, Mheshimiwa Rais aliwashukuru Wabunge hao kwa kuichagua Zanzibar kuwa moja ya sehemu yao ya kufanyia mikutano.
- 77. Mheshimiwa Spika**, katika kuimarisha uwekezaji, Mheshimiwa Dk. Ali Mohamed Shein Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, alikutana na Mwenyekiti wa Kampuni ya "Touchroad International Holdings Group" kutoka Jamhuri ya Watu wa China, Bwana He Liehui. Katika

mazungumzo yao, Mheshimiwa Rais alielezea historia ya ushirikiano baina ya Jamhuri ya Watu wa China na Zanzibar, ambao umetimia miaka 55. Kadhalika, Mheshimiwa Rais alisema kuwa, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inathamini mchango mkubwa katika kuziendeleza sekta mbali mbali za maendeleo unaotolewa na Jamhuri ya Watu wa China kwa Zanzibar, kutoka Serikali kuu, Taasisi na Makampuni ya Serikali na Binafsi.

**78. Mheshimiwa Spika,** kama ilivyo kawaida, Mheshimiwa Rais alijumuika na wafanyakazi katika maadhimisho ya Sherehe za Wafanyakazi za Mei Mosi 2019, ambazo mwaka huu zilifanyika katika Mkoa wa Kusini Unguja. Katika hotuba yake, Mheshimiwa Rais alisisitiza juu ya umuhimu wa uwajibikaji, uadilifu na utii wa sheria za kazi. Aliwataka wafanyakazi kutekeleza majukumu yao kwa misingi ya uzalendo na uwazi.

**79. Mheshimiwa Spika,** katika hotuba yake, Mheshimiwa Rais alielezea juhudi na mipango ya Serikali ya kuendelea kuimarisha maslahi ya wafanyakazi pamoja na mazingira ya kufanyia kazi kwa kadri hali ya uchumi inavyoendelea kuimarika. Kadhalika, Mheshimiwa Rais alielezea namna ambayo Serikali imejidhatiti katika kuimarisha uhusiano na ushirikiano na vyama vya wafanyakazi kupitia Shirikisho la Vyama Huru vya Wafanyakazi Zanzibar. Aidha, aliahidi kuyashughulikia maombi maalum yaliyotolewa na Uongozi wa Jumuiya ya

Vyama Huru vya Wafanyakazi na kuzishughulikia changamoto mbali mbali zilizowasilishwa.

- 80. Mheshimiwa Spika,** Tarehe 2 Mei, 2019, Mheshimiwa Rais alishiriki katika hafla ya uzinduzi wa majengo matatu ya Ofisi za Serikali yaliyoko Gombani Pemba. Majengo hayo mapya yenye vifaa vya kisasa ni ya aina yake na yatatumwa na Wizara sita za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Katika hotuba yake, alieleza kwamba ujenzi wa majengo hayo ni kielelezo cha mafanikio ya Serikali katika kuimarisha mazingira ya kufanyia kazi. Kadhalika, Mheshimiwa Rais alifahamisha kwamba hatua hio ni katika utekelezaji wa majukumu ya Serikali kama ilivyoelezwa katika Katiba ya Zanzibar ya Mwaka 1984 na utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi Mkuu wa CCM ya mwaka 2015-2020.
- 81. Mheshimiwa Spika,** kama kawaida, Mheshimiwa Rais alitoa risala ya kuukaribisha Mwezi Mtukufu wa Ramadhani kwa mwaka huu wa 2019 sawa na mwaka 1440 Hijriya. Katika nasaha zake, amewanasihi wafanyabiashara kuwa waadilifu na kuwafanyia wanunuzi tahfifu ya bei ya bidhaa na huduma zote zinazohitajika katika Mwezi Mtukufu wa Ramadhani. Aidha, aliongeza kusema kuwa kwa kufanya hivyo, hawatakula hasara bali watazidi kupata fadhila za Mola zinazoambatana na Mwezi huo.

- 82. Mheshimiwa Spika,** kadhalika, Mheshimiwa Rais amewahusia Waumini kuisoma Quran kwa wingi ndani ya Mwezi Mtukufu wa Ramadhani, kujitahidi kufahamu maelekezo yake pamoja na kuhudhuria madrasa ambazo huendeshwa katika misikiti mbali mbali. Aidha, katika risala yake alisisitiza haja ya wale wasiofunga kutokana na udhuru au wasio Waislamu, wauheshimu Mwezi huu kwa kutofanya mambo yanayoweza kuwaathiri waliofunga. Vile vile, Mheshimiwa Rais aliutakia kheri na mafanikio Mkutano wa 14 wa Baraza la Wawakilishi unaojadili Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha wa 2019/2020.
- 83. Mheshimiwa Spika,** uelewa wa wananchi juu ya shughuli zinazotekelezwa na Mheshimiwa Dk. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi umeongezeka kupitia utoaji wa taarifa kwa njia za kisasa za mawasiliano zikiwemo mitandao ya kijamii na tovuti ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Vile vile, taarifa zimetolewa kwa wananchi kupitia sinema katika Shehia mbali mbali za Unguja na Pemba. Hadi sasa idadi ya Shehia zilizofikiwa na sinema zetu Unguja na Pemba ni Shehia 15. Kiambatisho Nam. 2 kinatoa ufafanuzi zaidi. Katika Shehia zilizofikiwa, muitikio wa Wananchi ni mkubwa na wameonesha kufurahia sana zoezi hilo.

- 84. Mheshimiwa Spika**, vilevile, taarifa za kimaendeleo za vijiji na zile za utekelezaji wa mafanikio ya ahadi za Serikali zimekusanywa na kuripotwa kwa njia ya vipindi vya redio na televisheni pamoja na makala kupitia vyombo vya habari hapa nchini. Katika kipindi cha Julai – Machi, 2018/2019 vipindi 36 vimetayarishwa na kurushwa hewani kupitia Shirika la Utangazaji Zanzibar (Kiambatisho Nam. 3). Vipindi hivyo vimesheheni maoni ya wananchi katika kuelezea mafanikio ya utekelezaji wa miradi ya Serikali pamoja na changamoto ambazo zinawakabili katika maeneo yao.
- 85. Mheshimiwa Spika**, jumla ya nakala za kalenda 5,500 zimechapishwa zikielezea matukio mbali mbali yaliofanyika. Vile vile, matoleo ya jarida la Ikulu namba 38, 39, 40 na 41 ambayo ni sawa na nakala 12,000 yamechapishwa na kusambazwa katika Taasisi za Serikali, Taasisi Binafsi na Vituo vya Walimu Unguja na Pemba. Kadhalika, wananchi wa kawaida nao wamepatiwa jarida hili kupitia Ofisi za Masheha na mikusanyiko ya watu.
- 86. Mheshimiwa Spika**, ili kuongeza wigo wa mawasiliano na wananchi, sambamba na kuhakikisha kuwa taarifa za utekelezaji wa Mipango ya Serikali zinawafika wananchi wengi zaidi katika maeneo mbali mbali, ORMBLM imeanza mazungumzo na redio jamii za Unguja na Pemba kuangalia uwezekano wa kuvitumia vyombo hivyo katika kutoa taarifa. Nina furaha kuwaarifu

Waheshimiwa Wajumbe kwamba mazungumzo na redio hizo yamefikia hatua ya kuridhisha na ni matarajio yetu kwamba utekelezaji utanza muda mfupi ujao.

### **Programu ya Kuratibu Ushirikiano wa Kikanda, Mashirika ya Kimataifa na Wazanzibari Wanaoishi Nje ya Nchi**

- 87. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2018/2019, Programu hii iliidhinishiwa jumla ya TZS. milioni 537.9 kwa matumizi ya kazi za kawaida. Hadi kufikia mwezi Machi, 2019 Programu hii iliingiziwa jumla ya TZS. milioni 370.3 sawa na asilimia 69 kwa kazi za kawaida.
- 88. Mheshimiwa Spika,** utekelezaji wa programu hii umeiwezesha Zanzibar kuimarisha ushiriki wake katika Jumuiya za Mtangamano wa Kikanda za EAC, SADC, IORA na Utatu wa EAC-SADC-COMESA. Vile vile, umeimarisha uratibu wa Wanadiaspora wa Zanzibar kuendelea kushirikiana na Serikali na kuitikia wito na kuunga mkono jitihada za Serikali katika kuleta maendeleo ya nchi yao ya asili katika nyanja za Kiuchumi na Kijamii.
- 89. Mheshimiwa Spika,** Mkutano wa ishirini wa Kilele wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) ulifanyika Jijini Arusha tarehe 01 Februari, 2019. Mkutano huo ulijadili na kukubaliana mambo mbali mbali ya maendeleo ya Kiuchumi, Kisiasa, Usalama na



Kijamii. Miongoni mwa ajenda zilizojadiliwa ni kuundwa kwa Kamati ya Wataalamu wa Katiba (Constitutional Experts) kwa hatua za awali za kutayarisha Katiba ya Shirikisho la Kisiasa (Political Confederation) la Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kamati hio pia inajumuisha mjumbe kutoka Zanzibar. Vile vile, mkutano huo ulipitia Mkataba ulioanzisha Benki ya Maendeleo ya Afrika Mashariki, ili kuendana na muundo wa Jumuiya hiyo.

**90. Mheshimiwa Spika,** taarifa ya tathmini ya nchi ya Somali kujiunga na Jumuiya ya Afrika Mashariki iliwasilishwa na kujadiliwa. Wajumbe wa Mkutano huo walikubaliana kuwa Sekretarieti ikamilishe kazi ya kuitathmini Nchi hiyo kabla ya kuwa Mwanachama wa Jumuiya hio. Mkutano pia ulijadili na kuridhia Mswada wa Sheria ya Taasisi ya Fedha ya mwaka 2018 (the EAC Monetary Institute Bill, 2018) na Mswada wa Sheria ya Viapo ya mwaka 2018 (the EAC Oaths Bill, 2018). Kadhalika, Mkutano huo ulijadili Mkakati wa kuimarisha Viwanda vya Kuunganisha Magari (Assembly) kwa nia ya kupunguza uingizaji wa magari yaliotumika katika Nchi Wanachama.

**91. Mheshimiwa Spika,** ajenda nyengine zilizojadiliwa ni namna ya kuharakisha mapitio ya Sera za uingizaji bidhaa za Nchi Wanachama (EAC) na kuzioanisha kwa ajili ya kurahisisha utaratibu wa uingizaji bidhaa baina ya nchi hizo.

Lengo kuu likiwa ni kuunga mkono mpango wa kuimarisha viwanda vya ndani, ili kuvifanya kuwa imara na vyenye ushindani dhidi ya bidhaa za nje. Vile vile, Nchi Wanachama wamekubaliana kubadilisha muundo wa Jumuiya na kuwa na Naibu Katibu Wakuu wawili badala ya Muundo wa sasa unaoruhusu kila Nchi Mwanachama kuwa na Naibu Katibu Mkuu katika Jumuiya hio.

**92. Mheshimiwa Spika,** katika Mkutano wa majadiliano ya Mapitio ya Ushuru wa Pamoja wa Forodha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki uliyofanyika Kigali, Rwanda tarehe 26 Februari hadi 02 Machi, 2019; Zanzibar iliweza kuwasilisha mapendekezo yake ya kuzingatiwa na vikao hivyo kupitia Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa bidhaa zake muhimu za Mchele, Sukari na Unga wa Ngano. Aidha, zao la Karafuu nalo lilipewa nafasi yake na kupendekezwa kuingizwa kuwa miongoni mwa bidhaa nyeti kwa ajili ya kulinda zao hilo kwa uchumi wa nchi yetu. Zanzibar imeteuwa timu ya wataalamu wanne kushiriki mikutano hiyo ikiwa ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**93. Mheshimiwa Spika,** Jumuiya ya Afrika Mashariki imeendelea kuzitangaza na kuzitafutia masoko ya uhakika ya ndani na nje kwa bidhaa zinazozalishwa na wajasiriamali katika Nchi Wanachama wa Jumuiya hiyo kupitia Maonesho ya 19 ya JuaKali/ Nguvukazi yaliofanyika katika mji wa Eldoret, Kenya kuanzia tarehe 2 hadi 10 Disemba,

2018. Katika maonesho hayo Wajasiriamali 45 kutoka Zanzibar walishiriki na kutangaza bidhaa zinazozalishwa Zanzibar. Bidhaa hizo zilipendwa sana na kusifiwa kwa kuwa na viwango vilivyo bora na kufungashwa kwa weledi mkubwa.

**94. Mheshimiwa Spika,** Zanzibar imeendelea kushiriki katika Mikutano ya Jumuiya ya kikanda ya SADC kupitia programu zake mbali mbali za kuwaletea maendeleo Wananchi wa ukanda huu. Mikutano hiyo ni pamoja na Mkutano wa Baraza la Mawaziri la SADC lenye dhamana ya kuangalia masuala ya Bajeti na Miradi ulifanyika tarehe 11 hadi 17 Machi, 2019. Mkutano huo ulifanyika Windhoek, Namibia.

**95. Mheshimiwa Spika,** miongoni mwa mambo yaliojadiliwa katika Mkutano wa Baraza la Mawaziri ni pamoja na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa Mwenyekiti wa SADC kwa kipindi cha mwaka mmoja kinachoanza mwezi Agosti, 2019 hadi Agosti, 2020. Kwa mantiki hiyo, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itakuwa mwenyeji wa Mkutano wa Kilele wa Wakuu wa Nchi na Serikali utakaofanyika Jijini Dar es Salaam mwezi Agosti, 2019. Napenda kuliarifu Baraza lako Tukufu kuwa katika kipindi hicho tutashuhudia baadhi ya mikutano ya Jumuiya hiyo kufanyika hapa Zanzibar. Hali hii itapelekea Zanzibar kunufaika kiuchumi na kutangaza vivutio vya utalii vilivyopo nchini. Kamati za Kitaalamu na Kisera zinazojumuisha

wajumbe kutoka Zanzibar na Tanzania Bara tayari zimeundwa, ili kufanikisha jukumu hilo la Kitaifa na Kikanda.

- 96. Mheshimiwa Spika,** majadiliano ya Mkutano huo pia yalihusu utekelezaji wa mabadiliko ya kitaasisi ya Umoja wa Afrika katika maeneo makuu matano. Katika mabadiliko hayo ya Kitaasisi, Umoja wa Afrika umesisitiza lengo lake la kuzifanya nchi za Afrika kununua bidhaa zinazozalishwa ndani ya Afrika. Vile vile, ajenda nyengine iliojadiliwa ni Azimio la kufanya Mkutano wa mshikamano kuhusu Jamhuri ya Kidemokrasia ya Saharawi.
- 97. Mheshimiwa Spika,** ajenda nyengine zilizokuwa sehemu ya majadiliano hayo ni taarifa ya maandalizi ya Dira ya SADC (SADC Vision 2050) na Mapitio ya Mpango Mkakati wa Maendeleo wa SADC (Regional Indicative Strategic Plan 2015-2020); Taarifa ya awali ya utekelezaji wa Mkakati wa Viwanda wa SADC na Mpango kazi wake ambao umejumuisha maeneo makuu manne ikiwemo uendelezaji Viwanda, kuimarisha Ushindani, Mtangamano wa Kikanda na Masuala Mtambuka.
- 98. Mheshimiwa Spika,** vile vile, Mkutano wa Baraza la Mawaziri ulijadili pendekezo la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania la kuifanya lugha ya Kiswahili kuwa moja ya lugha rasmi na ya kazi ya Jumuiya ya SADC. Kwa sasa Jumuiya ya SADC

inatumia lugha tatu nazo ni Kiingereza, Kifaransa na Kireno. Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itawasilisha Andiko la Awali (Concept Paper) mwezi Juni, 2019 katika Sekretarieti ya SADC kuhusu uingizaji wa lugha ya Kiswahili. Hivyo, muda muafaka umefika wa nchi yetu kujipanga kuchangamkia fursa zitokanazo na lugha ya kiswahili ndani ya ukanda wa nchi za SADC.

**99. Mheshimiwa Spika,** kadhalika, Mkutano huo wa Baraza la Mawaziri la Jumuiya ya SADC ulijadili ajenda maalum ya utekelezaji wa Mpango wa kujitathmini Kiutawala Bora Barani Afrika (African Peer Review Mechanism, APRM) kwa kanda ya SADC. Nchi Wanachama wa SADC zinazotekeleza mpango huo kwa sasa ni Msumbiji, Afrika Kusini, Zambia, Mauritius na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Katika Mkutano huo Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilipata fursa ya kuwasilisha taarifa ya Utekelezaji wa mpango wake huo. Vilevile, taarifa ya APRM ya SADC, iliisifia Zanzibar kwa uweledi wake wa kukabiliana na changamoto za kisiasa kwa kuunda Serikali ya Umoja wa Kitaifa na kufanikiwa kukabiliana na maradhi ya Malaria kwa wananchi wake.

**100. Mheshimiwa Spika,** Mkutano wa Wataalamu na Mawaziri wa Nchi Wanachama wa Umoja wa Afrika wa kuanzisha eneo huru la biashara Barani Afrika ulifanyika tarehe 26 hadi 30 Novemba, 2018 Addis Ababa, Ethiopia na tarehe 13 Disemba, 2018 Cairo,

Misri. Lengo kuu la Mkutano huo ni kuendeleza majadiliano miongoni mwa Nchi Wanachama juu ya juhudi za Umoja wa Afrika katika kuanzisha eneo huru la biashara. Katika Mkutano huo Ujumbe wa Zanzibar ulioshiriki uliongozwa na Waziri wa Biashara na Viwanda Mheshimiwa Balozi Amina Salum Ali. Mkutano huo ulizungumzia kukamilika kwa itifaki mbali mbali za kuanzisha eneo huru la biashara ikiwemo kanuni ya uasili wa bidhaa.

**101. Mheshimiwa Spika,** Jumuiya ya Mashirikiano ya Bahari ya Hindi (IORA) iliendesha shughuli mbali mbali kwa ajili ya kuimarisha maendeleo endelevu ya nchi zilizopitiwa na Bahari ya Hindi. Maeneo yaliotiliwa nguvu zaidi katika majadiliano ya mikutano ya Jumuiya hiyo ni kuimarisha uchumi unaotokana na Bahari (Blue Economy) pamoja na miradi yake ikiwemo mradi wa zao la Mwani uliopendekezwa na Zanzibar. Mkutano wa Makatibu Wakuu wa Nchi Wanachama ulifanyika nchini Afrika Kusini tarehe 30 hadi 31 Julai, 2018 katika miji ya Durban na Johannesburg. Ujumbe wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Mikutano hio uliongozwa na Dkt. Islam Seif Salum, aliyekuwa Naibu Katibu Mkuu mwenye dhamana ya Uvuvi na Mifugo katika Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi Zanzibar.

**102. Mheshimiwa Spika,** Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imekuwa na mashirikiano mazuri na Wazanzibari wanaoishi nje ya nchi. Kwa miaka

mitatu mfululizo Serikali imekuwa ikiandaa Makongamano ya Wanadiaspora wa Tanzania wanaoishi nchi mbalimbali Duniani. Kongamano la Tano la Wanadiaspora wa Tanzania lilifanyika tarehe 18 na 19 Agosti, 2018 kwa mara ya kwanza katika Kisiwa cha Pemba. Kongamano hilo lilikuwa na Dhamira "Diaspora na Maendeleo" na Kauli Mbiu yake ilikuwa "Mtu Kwao Ndio Ngao". Kongamano hilo lilifunguliwa na Mheshimiwa Dk. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

**103. Mheshimiwa Spika,** kupitia Kongamano hilo, Wanadiaspora walishuhudia amani na utulivu kisiwani humo pamoja na kuimarika huduma za kijamii za hospitali, elimu na miundombinu ya Barabara. Aidha, Wanadiaspora hao walipata fursa ya kutembelea maeneo ya vivutio vya utalii na kujionea fursa za uwekezaji zilizopo Kisiwani Pemba. Hali hiyo imewapa faraja Wanadiaspora na kuahidi kuendelea kuwa Mabalazi wazuri wa nchi yao ya asili katika nchi wanazoishi.

**104. Mheshimiwa Spika,** kwa upande mwengine, Jumuiya ya Watanzania wanaoishi nchini Marekani waliandaa Mkutano wao wa mwaka (DICOTA Convention, 2018) uliofanyika tarehe 29 Agosti hadi 02 Septemba, 2018 nchini Marekani katika Jimbo la Washington – Seattle. Katika Mkutano huo uliofunguliwa na aliekuwa Waziri wa Katiba na Sheria wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Mheshimiwa Prof. Palamagamba John Kabudi na kufungwa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Issa Haji Ussi Gavu.

**105. Mheshimiwa Spika,** Ubalozi wa Tanzania Nchini Sweden kwa kushirikiana na Tanzania Diaspora Council - Global na Taasisi ya Swedish Sub Saharan Africa Chamber of Commerce waliandaa Kongamano la uwekezaji na uzinduzi wa Baraza la Watanzania Duniani uliofanyika tarehe 9 hadi 11 Aprili, 2019 nchini Sweden. Kongamano hilo lenye kauli mbiu ya Kuunganisha Wawekezaji na fursa zilizopo, lilifanyika kwenye Meli ya kitalii ya Tallink inayofanya safari zake kati ya Stockholm Sweden na Tallink Estonia. Mgeni rasmi wa Kongamano hilo alikuwa ni Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Job Ndugai. Zanzibar ilipata fursa ya kutoa mada ya fursa za uwekezaji Zanzibar na Uzoefu wa Zanzibar katika Sera ya Diaspora, zilizotolewa na Katibu Mkuu Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Ndugu Salum Maulid Salum.

**106. Mheshimiwa Spika,** kiujumla Wanadiaspora wamefarajika na ushiriki na utayari wa Serikali zetu mbili katika kuwaunganisha Diaspora wa Tanzania waliopo nchi mbali mbali. Kupitia Makongamano hayo, Wanadiaspora wamepata nafasi ya kuelewa fursa za uwekezaji, biashara na utalii katika nchi yao ya asili. Vile vile wameahidi kuwa watakuwa



Mabalozi wazuri wa kuwahamasisha wawekezaji na Wanadiaspora wa Tanzania katika Mataifa mbali mbali wanayoishi kuzitumia fursa hizo na kutembelea Tanzania.

**107. Mheshimiwa Spika,** kwa upande wao Wanadiaspora wameendelea kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika maeneo mbali mbali. Kwa mfano mwezi Septemba, 2018 timu ya madaktari kutoka Maryland, Marekani kupitia Jumuiya ya "Head INC" ilifika Zanzibar kwa mara ya tatu na kutoa huduma za matibabu pamoja na vifaa tiba. Huduma hizo zilitolewa katika Hospitali ya Wilaya iliyopo Kijiji cha Makunduchi Mkoa wa Kusini Unguja na Hospitali ya Wilaya iliyopo Kijiji cha Kivunge Mkoa wa Kaskazini Unguja.

**108. Mheshimiwa Spika,** miongoni mwa huduma zilizotolewa na madaktari hao ni matibabu ya maradhi ya ngozi, meno, maradhi ya wanawake, watoto, shinikizo la damu, kisukari pamoja na kutoa huduma za macho na kuwapatia miwani wagonjwa wote waliofika hapo wakiwa na matatizo ya macho yaliyohitaji miwani. Kadhalika, Wagonjwa wengine walifanyiwa operesheni ya macho na wengine walipewa dawa. Katika huduma hizo Wananchi walijitokeza kwa wingi kwa lengo la kupatiwa matibabu hayo pamoja na kutoa maoni yao kuhusu kuongezwa siku za kupatiwa huduma hizo.

**109. Mheshimiwa Spika,** Jumuiya ya Wazanzibari wanaoishi nchini Canada (ZACADIA) wamechangia vifaa vya afya kwa ajili ya watu wenye ulemavu. Vile vile, Jumuiya hio ilitoa msaada wa vitabu vya aina mbali mbali kwa Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA), Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Karume (KIST), Chuo cha Kilimo Kizimbani na Chuo cha Utawala wa Umma Zanzibar (IPA). Kadhalika, Wanadiaspora wa nchini Denmark (AHAS Group) wamechangia vifaa vya elimu na afya. Vifaa vya elimu vilipelekwa Skuli ya Msingi Kidongo Chekundu, Unguja na vifaa vya afya vilipelekwa Hospitali ya Mnazi Mmoja na Kivunge.

### **Programu ya Utumishi na Uendeshaji wa Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi**

**110. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2018/2019, Programu hii iliidhinishiwa jumla ya TZS. milioni 2,935.4 kwa matumizi ya kazi za kawaida. Hadi kufikia mwezi Machi, 2019 iliingiziwa TZS. milioni 1,898.1 sawa na asilimia 65 kwa kazi za kawaida.

**111. Mheshimiwa Spika,** utekelezaji wa programu hii umepelekea Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kupata mafanikio makubwa katika kuimarisha mazingira ya kufanya kazi kwa kuwapatia watumishi stahiki zao, kuimarisha utafiti na usalama wa Serikali.

- 112. Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai - Machi, 2018/2019 Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi imeendelea kuwajengea uwezo wafanyakazi kwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi. Jumla ya wafanyakazi 15 walipatiwa mafunzo ya muda mrefu kwenye ngazi za Stashahada, Shahada, Shahada ya Uzamili na Shahada ya Uzamivu. Kadhalika, wafanyakazi 224 wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi kama inavyoonekana katika Kiambatisho Nam. 4. Kati ya hao wafanyakazi 18 wamepatiwa mafunzo ya Programu maalum ya Usimamizi na Ukarimu yaliyotolewa kwa mashirikiano ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China kupitia Chuo cha "National Research Institute of Food and Fermentation Industries".
- 113. Mheshimiwa Spika,** kwa upande mwengine, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi imeendelea na utaratibu wa kuimarisha afya za wafanyakazi wake wakiwa kazini. Katika kufanikisha hilo, ORMBLM kwa kushirikiana na Wizara ya Afya wameendesha zoezi la kupima afya kwa wafanyakazi kwa maradhi yasiyoambukiza ambapo jumla ya wafanyakazi 94 walishiriki katika kupima afya zao. Vile vile, wafanyakazi hao walipatiwa taaluma ya kujikinga na maradhi hayo. Matokeo ya mafunzo hayo, yamepelekea wafanyakazi kufanya mazoezi kwa utaratibu unaofaa na kuepuka kula vyakula vinavyochangia kuongezeka kwa maradhi hayo.

- 114. Mheshimiwa Spika,** Kamati ya Uongozi na Kamati Tendaji Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi imefanya vikao vyake sita kwa mujibu wa Sheria inavyoelekeza. Vikao hivyo vilijadili na kutathmini utendaji kazi na kupitisha mpango wa manunuzi na mpango wa ukaguzi wa hesabu za ndani kwa mwaka wa fedha 2018/2019. Vile vile, Wafanyakazi 92 walipatiwa stahiki za likizo (Kiambatisho Nam. 5) kinatoa ufafanuzi. Kadhalika, wafanyakazi sita wamepatiwa mafao yao ya kustaafu.
- 115. Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi imeandaa Sera ya Mawasiliano na Habari ya ORMBLM. Sera hii inatarajiwa kuimarisha utaratibu wa Mawasiliano na utoaji wa taarifa. Kadhalika, inaelezea namna ya ukusanyaji na usimamizi wa habari zinazotolewa na ORMBLM. Vile vile, imeelezea namna ya ushirikishwaji wa wananchi wakati wa utoaji na upokeaji wa taarifa utakavyofanyika na inasisitiza haja ya kuzingatia maadili wakati wa utoaji na upokeaji wa habari.
- 116. Mheshimiwa Spika,** ORMBLM ipo katika hatua za mwisho za kukamilisha tafiti mbili ambazo ni Utafiti juu ya fursa zinazopatikana katika Jumuiya ya Afrika Mashariki na namna Zanzibar itakavyonufaika na fursa hizo na Utafiti juu ya mahitaji ya kufundisha na kujifunza Kiswahili kwa nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Tafiti hizo zimefanywa kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA). Tafiti zote mbilizimebainisha wazi fursa zinazopatikana katika Jumuiya ya Afrika Mashariki na namna Zanzibar itakavyonufaika nazo. Fursa hizo ni pamoja na kuongezeka masoko kwa bidhaa zinazozalishwa ndani ya nchi, kuongezeka fursa katika Sekta ya utalii, fursa katika ujenzi wa Bandari na Uwanja wa ndege, kusafirisha bidhaa, fursa za kielimu na fursa kwa upande wa mafuta na gesi.

**117. Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa mradi wa maendeleo, ujenzi wa Ikulu ndogo ya Micheweni umekamilika. Kadhalika, ujenzi wa Jengo jipya la Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Chake Chake Pemba unaendelea. Ujenzi huo unatarajiwa kukamilika katika mwaka wa fedha wa 2019/2020. Vile vile, utaratibu wa kumpata Mkandarasi wa kuzuia mmong'onyoko wa udongo katika Ikulu ndogo ya Mkoani umekamilika na hatua za ujenzi zitaanza kabla ya kumalizika mwaka huu wa bajeti.

**118. Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai – Machi, 2018/2019 watumishi 2,113 wamefanyiwa upekuzi wa awali na endelevu na Ofisi ya Usalama wa Serikali (Kiambatisho Nam. 6) kinahusika. Kwa upande mwengine, Ofisi ya Usalama wa Serikali imefanya ukaguzi wa kiusalama wa majengo na miundombinu muhimu ya Serikali kama inavyoonekana katika Kiambatisho Nam.

7. Matokeo ya ukaguzi huo yameonesha kuwa watumishi wa Serikali wanafanya kazi katika mazingira salama kutokana na kufanyiwa kazi mapendekezo yanayotolewa kila baada ya ukaguzi kukamilika.

**119. Mheshimiwa Spika,** uelewa wa watumishi wa Serikali juu ya utunzaji wa siri za Serikali umeendelea kuimarika kufuatia kuendelea kutolewa kwa mafunzo juu ya udhibiti wa siri na utunzaji wa nyaraka za Serikali yanayotolewa. Jumla ya watumishi 671 kutoka Taasisi mbali mbali wamepatiwa mafunzo hayo kama inavyoonekana katika Kiambatisho Nam. 8.

**120. Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi - Pemba imeendelea kutekeleza majukumu yake kwa kushirikiana na Ofisi na Idara nyengine za ORMBLM. Katika kipindi hiki, iliratibu ziara alizofanya Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Kisiwani Pemba. Ziara hizo ni ziara ya kushiriki Kongamano la Tano la Diaspora Tanzania, Siku ya Wanawake, Maadhimisho ya Siku ya Chakula Duniani, Maadhimisho ya Sherehe za Mapinduzi, Siku ya Sheria, ziara za Wilaya na Ufunguzi wa Jengo la Ofisi za Serikali Pemba. Kadhalika, Vikao tisa vya Maofisa Wadhamini vimefanyika kwa ufanisi mkubwa. Katika vikao hivyo, mada mbali mbali zilijadiliwa ikiwa ni pamoja na ushirikiano katika kazi, uadilifu na matumizi mazuri ya rasilimali.

## **Programu ya Usimamizi wa Majukumu ya Kikatiba na Kisheria ya Baraza la Mapinduzi na Kamati ya Makatibu Wakuu**

- 121. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2018/2019, Programu hii iliidhinishiwa TZS. milioni 509.8. Hadi kufikia mwezi Machi, 2019 iliingiziwa TZS. milioni 347.2 sawa na asilimia 68 kwa kazi za kawaida.
- 122. Mheshimiwa Spika,** kupitia Programu hii, mafanikio makubwa yamepatikana ikiwemo kufanikisha vikao vya Baraza la Mapinduzi na Kamati zake pamoja na Kamati ya Kitaalamu ya Makatibu Wakuu. Jumla ya vikao 35 vya Baraza la Mapinduzi vilifanyika ambavyo pamoja na mambo mengine vilijadili nyaraka mbali mbali za Sheria na Sera (Kiambatisho Nam. 9) kinatoa ufafanuzi. Vile vile, vikao 21 vya Kamati ya Makatibu Wakuu navyo vilifanyika kwa wakati. Katika vikao hivyo, nyaraka za Sheria na Sera zilitolewa maoni ya kitaalamu na kuwasilishwa katika Baraza la Mapinduzi kwa ajili ya kufanyiwa maamuzi.
- 123. Mheshimiwa Spika,** naomba kuliarifu Baraza lako Tukufu kuwa ORMBLM kupitia Baraza la Mapinduzi iliendelea na utaratibu wake wa kutoa mafunzo ya kuwajengea uwezo Viongozi na Watendaji Wakuu wa Serikali. Kazi hio imekuwa ikifanywa kwa kushirikiana na wataalamu kutoka Taasisi mbali mbali za hapa Tanzania. Mafunzo

hayo yanatolewa katika nyanja za Utawala Bora, Usimamizi wa Rasilimali na Matumizi ya Ushahidi wa Kisayansi katika kufanya Maamuzi na kuandaa Sera.

**124. Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2018/2019, Mheshimiwa Dk. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi aliongoza Kongamano la Viongozi wa Kisiasa na Watendaji Wakuu wa Serikali katika kujadili usimamizi mzuri na matumizi sahihi ya Ardhi na Rasilimali zisizorejesheka nchini. Kongamano hilo lilifanyika tarehe 16 Machi, 2019 katika ukumbi wa Sheikh Idris Abdul – Wakil. Mada mbali mbali ziliwasilishwa katika Kongamano hilo zikiwemo (i) Sheria zinazosimamia matumizi ya ardhi Zanzibar; (ii) Hali ya maendeleo ya rasimali za misitu na changamoto zake; (iii) Hali halisi ya maliasili zisizorejesheka Zanzibar; na (iv) Hali ya mchanga Zanzibar na mwelekeo wake.

**125. Mheshimiwa Spika**, mafunzo mengine yalitolewa yalikuwa ni kuhusu Matumizi ya Ushahidi wa Kisayansi katika kufanya Maamuzi na kuandaa Sera (Evidence Based Policy). Lengo la mafunzo hayo lilikuwa ni kuwajengea uwezo watendaji wa Serikali, ili waweze kupanga na kutekeleza mipango ya Serikali pamoja na kusaidia katika kufanya maamuzi ya kisera kwa kutumia ushahidi uliopo. Mafunzo hayo yalitolewa kwa Makatibu Wakuu, Wakurugenzi Mipango, Sera na Utafiti



na watendaji wengine wa Serikali. Mafunzo hayo yalifanyika kwa ushirikiano na Taasisi ya Sayansi na Teknolojia Tanzania (COSTECH) yenye Makao Makuu yake jijini Dar es Salaam.

**126. Mheshimiwa Spika,** kwa upande mwengine, Makatibu na Manaibu Makatibu Wakuu walipatiwa mafunzo kuhusu usimamizi mzuri wa masuala ya fedha. Mafunzo hayo yalifanyika tarehe 21 Agosti, 2018 katika Ukumbi wa Hoteli ya Verde. Vile vile, Wakurugenzi na Maofisa Sera na Utafiti wamejengewa uwezo juu ya masuala ya Sera, Ufuatiliaji na Tathmini kwa kutumia Moduli ya "Result Based Management". Lengo la mafunzo hayo ni kukuza uelewa kwa Wakurugenzi na Maofisa juu ya kufanya tafiti na kufahamu mbinu zinazotumika katika kufanya Ufuatiliaji na Tathmini. Mafunzo hayo yaliendeshwa kwa kushirikiana na UONGOZI INSTITUTE ya Dar es Salaam.

**127. Mheshimiwa Spika,** napenda kuliarifu Baraza lako Tukufu kuwa Kitengo cha Ufuatiliaji na Tathmini kimeanza kazi rasmi kwa kuandaa viashiria vinavyoweza kupima matokeo halisi ya shughuli zinazotekelezwa na kupangiwa fedha kwa mujibu wa vipaumbele vya Wizara za Serikali. Vile vile, Kitengo kilifuatilia utekelezaji wa masuala maalum yanayohusu Sera, Sheria, na maamuzi kwa Wizara 15 za SMZ na kuandaa Ripoti ya Utekelezaji wa Maamuzi na Maagizo ya Serikali kwa Taasisi hizo.

**128. Mheshimiwa Spika,** kwa upande mwengine, Kitengo cha Ufuatiliaji na Tathmini kimekamilisha kufanya tathmini ya hali ya upatikanaji wa huduma ya maji katika Mkoa wa Mjini Magharibi na kutoa ripoti ambayo inaendelea kufanyiwa kazi. Kadhalika, Kitengo kimeanza kufanya tathmini kuhusu upatikanaji wa pembejeo za kilimo ambayo imepangwa kukamilika mwezi Julai, 2019.

### **Programu ya Utumishi na Uendeshaji wa Ofisi ya Baraza la Mapinduzi**

**129. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2018/2019, Programu hii iliidhinishiwa jumla ya TZS. milioni 1,451.8. Hadi kufikia mwezi Machi, 2019 Programu hii iliingiziwa TZS. milioni 1,041.4 sawa na asilimia 72 kwa kazi za kawaida.

**130. Mheshimiwa Spika,** mafanikio yaliyofikiwa kutokana na utekelezaji wa Programu hii ni pamoja na kuimarika mazingira ya kazi. Uwezo wa watumishi umeendelea kuimarika na kuwa wenye ufanisi zaidi kutokana na kuendeleza programu za kujenga uwezo wao wa kitaaluma kwa mafunzo ya muda mfupi na mrefu kulingana na mahitaji na mabadiliko ya wakati.

**131. Mheshimiwa Spika,** hadi hivi sasa, watumishi wanne wanaendelea kupatiwa mafunzo ya muda mrefu katika ngazi za shahada ikiwemo ya Sayansi ya Habari na Ununuzi na Ugavi. Wafanyakazi watatu

wanapatiwa mafunzo ya stashahada ya uzamili katika fani za Uongozi, Utafiti wa Sera za Umma na Sayansi ya Kompyuta. Vile vile, Wafanyakazi wengine sita wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi katika fani za Itifaki, Usimamizi wa Fedha, Udereva wa Viongozi Mashuhuri. Sambamba na hilo Wafanyakazi wamepatiwa taaluma ya namna ya kujikinga na maradhi yasiyoambukiza na yanayoambukiza.

### **3. MWELEKEO WA BAJETI YA OFISI YA RAIS NA MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020**

**132. Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa mwaka wa fedha 2019/2020 itaendelea kutekeleza Programu Kuu tano na Programu Ndogo 11.

**133. Mheshimiwa Spika,** bajeti ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa mwaka wa fedha 2019/2020 kwa Fungu A01 na A02 ni jumla ya TZS. milioni 11,726.5 zikijumuisha mishahara, matumizi ya kawaida na mradi wa maendeleo. Bajeti hii kwa upande wa matumizi ya kawaida imeongezeka kutoka TZS. milioni 4,830.8 hadi TZS. milioni 5,063.4. Ongezeko hilo ni la TZS. milioni 232.6 sawa na asilimia 5 ya ongezeko. Kwa upande wa mradi wa maendeleo imeongezeka kutoka TZS. milioni 1,000.0 hadi TZS. milioni 2,000.0 sawa na asilimia 100 ya ongezeko. Ongezeko hili ni

kutokana kuongezeka kwa mahitaji ya kuimarisha nyumba za Ikulu.

**134. Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa mwaka wa fedha wa 2019/2020 imejipangia kutekeleza vipaumbele vifuatavyo:-

- i. Kuratibu shughuli na kusimamia huduma za Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi,
- ii. Kusimamia majukumu ya Kikatiba na Kisheria ya Baraza la Mapinduzi na Kamati zake,
- iii. Kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa shughuli za Wizara, Idara na Taasisi za Serikali pamoja na maamuzi ya Serikali,
- iv. Kuendelea kuelimisha Viongozi na jamii juu ya Sera ya Diaspora ya Zanzibar,
- v. Kuwajengea uwezo Viongozi na Watendaji katika kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi,
- vi. Kuwawezesha wananchi kupata taarifa juu ya utekelezaji wa shughuli za Serikali yao,
- vii. Kuratibu ushiriki wa watendaji wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika vikao vya mtangamano wa Jumuiya za Kikanda vyenye kuleta tija kwa Zanzibar,
- viii. Kuwashajihisha Wanadiaspora wa Zanzibari kuchangia katika maendeleo ya Zanzibar,
- ix. Kuimarisha mazingira na usalama katika nyumba za Ikulu, Unguja, Pemba, Dar es Salaam na Dodoma,

- x. Kuimarisha usalama kwa watumishi wa Serikali na maeneo wanayofanyia kazi, na
- xi. Kuimarisha mazingira ya kazi na kufanikisha utekelezaji wa shughuli za Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

**135. Mheshimiwa Spika,** vipaumbele hivyo vitatekelezwa kupitia shughuli mbali mbali ambazo Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi imejipangia katika Mpango Kazi wake wa mwaka wa fedha 2019/2020 kama ifuatavyo:-

- i. Kuratibu shughuli za Mheshimiwa Rais,
- ii. Kusimamia huduma za Mheshimiwa Rais,
- iii. Kumalizia ujenzi wa Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Chake Chake Pemba,
- iv. Kuimarisha Maktaba ya Mheshimiwa Rais,
- v. Kukuza mawasiliano kupitia mitandao ya kijamii na kutathmini matumuzi ya TEHAMA katika ORMBLM,
- vi. Kuratibu shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na ushiriki wake katika mikutano ya Kikanda na Kimataifa,
- vii. Kujenga uwelewa juu ya fursa zinazopatikana kutokana na jumuiya za Mtangamano wa Kikanda, (EAC, SADC, IORA, TRIPATITE),
- viii. Kuendelea kujenga uelewa kwa jamii juu ya Sera ya Diaspora ya Zanzibar na utekelezaji wake,
- ix. Kufanya utafiti wa Ushiriki na tija kwa Zanzibar katika mikutano ya kikanda na Kimataifa kutoka 2015/2016 mpaka 2017/2018,

- x. Kufanya tathmini juu ya uelewa wa wafanyakazi wa Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kuhusu Sheria ya Utumishi wa Umma ya mwaka 2011 na Kanuni zake,
- xi. Kutoa elimu juu ya utunzaji wa siri za Serikali kwa watumishi wa umma,
- xii. Kufanya Ufuatiliaji na Tathmini ya Utendaji kazi wa Taasisi za Umma,
- xiii. Kukijengea Uwezo Kitengo cha Ufuatiliaji na Tathmini, na
- xiv. Kuimarisha Kitengo cha Uandaaji, Usambazaji na Uhifadhi wa Kumbukumbu za Baraza la Mapinduzi.

#### **4. PROGRAMU KUBWA NA NDOGO NA MAKISIO YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020**

**136. Mheshimiwa Spika,** Programu, vipaumbele na shughuli za Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi zitatekelezwa na Ofisi na Idara zifuatazo:-

- i. Ofisi ya Faragha ya Rais,
- ii. Ofisi ya Baraza la Mapinduzi,
- iii. Idara ya Mawasiliano na Habari Ikulu,
- iv. Idara ya Ushirikiano wa Kimataifa na Uratibu wa Wazanzibari Wanaoishi Nje ya Nchi,
- v. Idara ya Uendeshaji na Utumishi,
- vi. Idara ya Mipango, Sera na Utafiti,
- vii. Ofisi ya Usalama wa Serikali, na
- viii. Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi – Pemba.

**137. Mheshimiwa Spika,** Programu za Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Fungu A01 ni kama zifuatazo:-

**Programu ya Kuratibu Shughuli na Kusimamia Huduma za Mheshimiwa Rais na Kuimarisha Mawasiliano Ikulu**

**138. Mheshimiwa Spika,** lengo kuu la Programu hii ni kuratibu shughuli, kusimamia huduma za Mheshimiwa Rais na kuimarisha mawasiliano yatakayowawezesha wananchi kuendelea kupata taarifa za shughuli za kimaendeleo zinazotekelezwa na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa wananchi wake. Kadhalika, matokeo ya Programu hii ni kuendeleza taswira nzuri ya Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Programu hii itakuwa na Programu Ndogo mbili zifuatazo:-

- i. Programu Ndogo ya Kuratibu shughuli na kusimamia huduma za Mheshimiwa Rais, na
- ii. Programu Ndogo ya Kuimarisha Mawasiliano baina ya Serikali na Wananchi.

**139. Mheshimiwa Spika,** katika kufikia malengo ya programu hii, shughuli zifuatazo zimepangwa kutekelezwa:-

- i. Kuratibu shughuli za Mheshimiwa Rais,
- ii. Kutoa huduma za uendeshaji na utawala katika Ofisi za Washauri wa Mheshimiwa Rais,
- iii. Kuratibu shughuli ya kutunuku Nishani,

- iv. Kutoa huduma za uendeshaji na Utawala katika Ofisi ya Faragha ya Mheshimiwa Rais,
- v. Kuimarisha Maktaba ya Mheshimiwa Rais,
- vi. Kuwajengea uwezo wafanyakazi kwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi,
- vii. Kusimamia huduma katika nyumba za makaazi ya Mheshimiwa Rais katika Ikulu zilizopo Unguja, Pemba, Dar es Salaam na Dodoma,
- viii. Kukuza mawasiliano baina Wananchi na Wahusika wengine wa habari kupitia televisheni na redio,
- ix. Kutayarisha, kuchapisha na kusambaza majarida na machapisho maalum ya Ikulu, na
- x. Kuimarisha mawasiliano kupitia mitandao ya kijamii na kutathmini matumizi ya TEHAMA katika ORMBLM.

**140. Mheshimiwa Spika,** ili Programu ya Kuratibu Shughuli na Kusimamia Huduma za Mheshimiwa Rais na Kuimarisha Mawasiliano Ikulu iweze kutekelezwa, kwa mwaka wa fedha 2019/2020, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya TZS. milioni 4,174.3 kwa matumizi ya kazi za kawaida zilizopangwa katika Programu hii.



## **Programu ya Kuratibu Ushirikiano wa Kikanda, Mashirika ya Kimataifa na Wazanzibari Wanaoishi Nje ya Nchi**

141. Mheshimiwa Spika, lengo kuu la Programu hii ni kuimarisha kuendeleza ushiriki wa Zanzibar katika mikutano ya Jumuiya za Kikanda, Kimataifa na Kuwashirikisha ipasavyo Wazanzibari wanaoishi nje ya Nchi katika maendeleo ya Kiuchumi na Kijamii ya nchi yao ya asili. Kadhalika, matokeo ya utekelezaji wa Programu hii ni kuendelea kufaidika kwa Zanzibar na fursa za Kiuchumi na Kijamii zinazotokana na Jumuiya za Kikanda, Kimataifa na Wazanzibari wanaoishi nje ya Nchi. Programu hii itakuwa na Programu Ndogo mbili zifuatazo:-
- i. Programu Ndogo ya Kuratibu Shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Kikanda na Kimataifa, na
  - ii. Programu Ndogo ya Kuratibu Shughuli za Wazanzibari Wanaoishi Nje ya Nchi.
142. **Mheshimiwa Spika**, katika kufikia malengo ya programu hii, shughuli zifuatazo zimepangwa kutekelezwa:-
- i. Kushiriki katika Mikutano ya Kikanda ndani ya nchi,
  - ii. Kushiriki katika Mikutano ya Kikanda nje ya nchi,
  - iii. Kusimamia shughuli za kila siku za Idara ya Ushirikiano wa Kimataifa na Uratibu wa Wazanzibari Wanaoishi Nje ya Nchi,

- iv. Kujenga uelewa juu ya fursa zinazopatikana kutokana na Jumuiya za mtangamano wa Kikanda (EAC, SADC, IORA, TRIPATITE na AU),
- v. Kujenga Ushirikiano wa Kimataifa,
- vi. Kujenga uelewa kwa jamii juu ya Sera ya Diaspora Zanzibar na utekelezaji wake,
- vii. Kuandaa Kongamano la Watanzania wanaoishi nje ya nchi, na
- viii. Kushiriki katika mikutano ya ndani na kimataifa inayohusiana na Diaspora.

**143. Mheshimiwa Spika,** ili Programu ya Ushirikiano wa Kimataifa na Uratibu wa Wazanzibari Wanaoishi Nje ya Nchi iweze kutekelezwa, kwa mwaka wa fedha 2019/2020, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya TZS. milioni 648.3 kwa matumizi ya kazi za kawaida zilizopangwa katika Programu hii.

### **Programu ya Utumishi na Uendeshaji wa Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi**

**144. Mheshimiwa Spika,** malengo makuu ya Programu hii ni kuimarisha uwezo wa kiutendaji na kuratibu shughuli za Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Kuimarisha Shughuli za Mipango, Kuandaa na Kuchambua Sera na Kufanya Utafiti, Kuimarisha Usalama wa Serikali na Kuratibu Shughuli za Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi - Pemba. Matokeo ya utekelezaji

wa Programu hii ni kuimarika kwa mazingira ya utendaji kazi pamoja na ufuatiliaji wa shughuli za ORMBLM. Programu hii itakuwa na Programu Ndogo nne zifuatazo:-

- i. Programu Ndogo ya Uratibu na Usimamizi wa Shughuli za ORMBLM,
- ii. Programu Ndogo ya Uratibu wa Shughuli za Mipango, Sera na Utafiti za ORMBLM,
- iii. Programu Ndogo ya Uratibu na Usimamizi wa Shughuli za ORMBLM – Pemba, na
- iv. Programu Ndogo ya Kusimamia Usalama wa Watumishi wa Umma.

**145. Mheshimiwa Spika,** Programu hii itatekelezwa sambamba na mradi wa ujenzi na Ukarabati wa nyumba za Ikulu.

**146. Mheshimiwa Spika,** katika kufikia malengo ya programu hii, shughuli zifuatazo zimepangwa kutekelezwa:-

- i. Kuandaa na kuratibu mikutano ya Kamati Tendaji na Kamati ya Uongozi ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi,
- ii. Kutoa huduma za Uendeshaji na Utawala katika Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi,
- iii. Kuwajengea uwezo wafanyakazi kwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi,
- iv. Kuendesha vikao vya Bodi ya Zabuni vya ORMBLM,

- v. Kufanya Ukaguzi wa hesabu za awali na endelevu na Vikao vya Kamati ya Ukaguzi,
- vi. Kufanya utafiti juu ya ushiriki na tija kwa Zanzibar katika mikutano ya Kikanda na Kimataifa,
- vii. Kuendelea na ujenzi wa jengo la ORMBLM – Pemba,
- viii. Kufanya matengenezo ya jengo la Ikulu ya Mnazi mmoja,
- ix. Kujenga nyumba ya kuhudumia Viongozi Wakuu Dodoma,
- x. Kuimarisha huduma katika Ikulu za Chake Chake, Mkoani na Micheweni,
- xi. Kutoa huduma za Uendeshaji na Utawala katika Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi – Pemba,
- xii. Kufanya Upekuzi wa Kiusalama wa awali na endelevu kwa wafanyakazi,
- xiii. Kufanya Ukaguzi wa Kiusalama wa Majengo na Miundombinu kwa majengo ya Serikali na
- xiv. Kuandaa Mafunzo na warsha juu ya utunzaji wa siri na udhibiti wa nyaraka kwa watumishi wa Serikali.

**147. Mheshimiwa Spika,** ili Programu ya Utumishi na Uendeshaji wa Ofisi Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi iweze kutekelezwa, kwa mwaka wa fedha 2019/2020, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya TZS. milioni 4,771.8 kwa matumizi ya kazi za kawaida zilizopangwa katika

Programu hii na jumla ya TZS. milioni 2,000.0 kwa ajili ya mradi wa maendeleo.

- 148. Mheshimiwa Spika,** Programu za Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Fungu A02 ni kama zifuatazo:-

**Programu ya Usimamizi wa Majukumu ya Kikatiba na Kisheria ya Baraza la Mapinduzi na Kamati ya Makatibu Wakuu**

- 149. Mheshimiwa Spika,** lengo la Programu hii ni kuhakikisha uwajibikaji wa Serikali katika kutoa huduma bora zinazohitajika kwa Wananchi. Aidha, kuhakikisha malengo ya Kitaifa, Wizara na Taasisi zake yanatekelezwa ipasavyo na kufikiwa kama yalivyotarajiwa. Matokeo ya utekelezaji wa Programu hii ni kuimarika kwa uwajibikaji, Sera, Sheria na Miongozo yenye kusaidia ukuaji wa uchumi, maendeleo na kudumisha amani na mshikamano wa wananchi. Program hii itakuwa na Programu Ndogo mbili zifuatazo:-

- i. Programu Ndogo ya Kuratibu na Kusimamia shughuli za Baraza la Mapinduzi na Kamati zake, na
- ii. Programu Ndogo ya Tathmini ya Utendaji kazi na Uwajibikaji wa Taasisi za Umma.

**150. Mheshimiwa Spika,** katika kufikia malengo ya programu hii, shughuli zifuatazo zimepangwa kutekelezwa:-

- i. Kutayarisha vikao vya kawaida vya Baraza la Mapinduzi na Kamati ya Makatibu Wakuu na kufuatilia utekelezaji wa maamuzi yake,
- ii. Kutayarisha vikao maalum vya Baraza la Mapinduzi na Kamati zake na kufuatilia utekelezaji wake,
- iii. Kusimamia programu za mafunzo ya kujenga uwezo wa watendaji wa Serikali na Sekretarieti ya Baraza la Mapinduzi,
- iv. Kuimarisha taswira na hali ya utumishi wa Umma nchini,
- v. Kuratibu kazi na ziara za Waheshimiwa Mawaziri wasiokuwa na Wizara maalum,
- vi. Kuandaa vikao vya kuhimiza uwajibikaji wa watumishi wa Umma kati ya Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi na Watendaji Wakuu wa Wizara na Taasisi za SMZ,
- vii. Kutayarisha mikutano kati ya Mheshimiwa Rais na Wizara za SMZ kutathmini utekelezaji wa Mipango kazi na kufuatilia utekelezaji wa maagizo na maelekezo yake,
- viii. Kufuatilia utekelezaji wa masuala maalum ya Sera, Sheria na maamuzi ya Serikali, na
- ix. Kuwajengea uwezo wa kiutendaji watumishi wa kitengo cha Ufuatiliaji na Tathmini.

**151. Mheshimiwa Spika**, ili Programu ya Usimamizi wa Majukumu ya Kikatiba na Kisheria ya Baraza la Mapinduzi na Kamati ya Kitaalamu ya Makatibu Wakuu iweze kutekelezwa kikamilifu, kwa mwaka wa fedha 2019/2020, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya TZS. milioni 592.4 kwa matumizi ya kazi za kawaida zilizopangwa katika Programu hii.

### **Programu ya Utumishi na Uendeshaji wa Ofisi ya Baraza la Mapinduzi**

**152. Mheshimiwa Spika**, lengo kuu la Programu hii ni kuimarisha mazingira utendaji kazi, mahusiano ya Umma na kuongeza ujuzi wa Wafanyakazi. Matokeo ya utekelezaji wa Programu hii ni kuwa na mfumo bora na wa kisasa wa kuendesha shughuli kwa ufanisi na uhifadhi wa Nyaraka na Kumbukumbu. Programu hii itakuwa na Programu Ndogo ifuatayo:-

- i. Programu Ndogo ya Utumishi na Uendeshaji wa Ofisi ya Baraza la Mapinduzi.

**153. Mheshimiwa Spika**, katika kufikia malengo ya programu hii, shughuli zifuatazo zimepangwa kutekelezwa:-

- i. Kuimarisha huduma za Maktaba na Kitengo cha uandaaji, usambazaji na uhifadhi wa kumbukumbu za Baraza la Mapinduzi,
- ii. Kuimarisha miundombinu ya majengo pamoja na mazingira yake,

- iii. Kuimarisha upatikanaji wa huduma za mawasiliano na utekelezaji wa kazi za kila siku,
- iv. Kutoa taaluma ya afya kuhusu maradhi yasiyoambukiza na kujikinga na VVU/ UKIMWI na
- v. Kutoa mafunzo ya muda mrefu na mfupi kwa wafanyakazi.

**154. Mheshimiwa Spika,** ili Programu ya Utumishi na Uendeshaji wa Ofisi ya Baraza la Mapinduzi iweze kutekelezwa kikamilifu, kwa mwaka wa fedha 2019/2020, naiomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya TZS. milioni 1,539.7 kwa matumizi ya kazi za kawaida zilizopangwa katika Programu hii.

## **5. MAOMBIYA FEDHA KWA KAZIZILIZOPANGWA KUTEKELEZWA KATIKA MWAKA WA FEDHA 2019/2020**

### **5.1 MATUMIZI YA KAWAIDA NA MIRADI YA MAENDELEO**

**155. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka 2019/2020, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi inakadiria kutumia jumla ya TZS. milioni 11,726.5 kwa ajili ya matumizi ya utekelezaji wa Programu za Fungu A01 na A02. Fungu A01 linakadiriwa kutumia TZS. milioni 9,594.4 kwa kazi za kawaida na mradi wa maendeleo. Kati ya fedha hizo jumla



ya TZS. milioni 7,594.4 kwa ajili ya kazi za kawaida na jumla ya TZS. milioni 2,000.0 kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa maendeleo. Fungu A02 linakadiriwa kutumia jumla ya TZS. milioni 2,132.1 kwa kazi za kawaida.

## **5.2 MAOMBI YA FEDHA 2019/2020**

- 156. Mheshimiwa Spika,** ili kuiwezesha Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kutekeleza kazi zilizopangwa kwa mwaka wa fedha 2019/2020, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha makadirio ya matumizi ya Programu za Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi yenye jumla ya TZS. milioni 11,726.5. Kati ya fedha hizo, TZS. milioni 9,726.5 kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida na TZS. milioni 2,000.0 kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Mgawanyo wa fedha zitakazotumika kwa utekelezaji wa kila Programu umeainishwa katika Kiambatisho Nam. 10.

## **6. HITIMISHO**

- 157. Mheshimiwa Spika,** kwa mara nyengine tena naomba kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dk. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa namna anavyotekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015 - 2020 kwa vitendo. Sote ni mashahidi kuwa mambo

mengi aliyoahidi kuyatekeleza katika kipindi hiki tayari ameshayatekeleza. Ameidhirishia Dunia kwamba “Muungwana ni vitendo”. Natoa wito kwetu sisi Wawakilishi wa wananchi tutekeleze ahadi tulizoahidi katika Majimbo yetu, ili tuungane na Mheshimiwa Rais wetu mpendwa katika kuwatumikia wananchi waliotuchagua na kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015 - 2020.

- 158. Mheshimiwa Spika**, mimi binafsi namshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kuniadini na kunipa dhamana hii. Naahidi kuwa muaminifu na mtiifu kwake na kuendelea kufanya kazi kwa ufanisi, uadilifu na uaminifu, ili kufikia malengo yaliyokusudiwa.
- 159. Mheshimiwa Spika**, nachukua fursa hii kuwapongeza kwa dhati wale wote tunaofanya kazi hizi kwa pamoja wakiwemo Dkt. Abdulhamid Yahya Mzee, Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi; Ndugu Salum M. Salum, Katibu Mkuu ORMBLM; Ndugu Haroub Shaib Mussa, Katibu wa Rais; Ndugu Salmin Amour Abdallah, Naibu Katibu Baraza la Mapinduzi; Ndugu Salum Kassim Ali, Naibu Katibu Mkuu ORMBLM; Ndugu Maryam Haji Mrisho, Naibu Katibu wa Rais; Dkt. Juma Yakout Juma, Naibu Katibu Msaidizi Baraza la Mapinduzi; Wakurugenzi na watumishi wengine. Aidha, nawapongeza Washauri wa Mheshimiwa Rais

ambao ni Mheshimiwa Chimbeni Kheir Chimbeni, Mheshimiwa Burhan Saadat Haji, Mheshimiwa Abdulrahman Mwinyi Jumbe, Mheshimiwa Zainab Omar Mohammed na Mheshimiwa Maua Abeid Daftari kwa wanavyotekeleza kazi zao za ushauri kwa uadilifu.

**160. Mheshimiwa Spika,** nawashukuru Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza lako Tukufu kwa kunisikiliza kwa umakini mkubwa wakati wote wa kuwasilisha Hotuba hii. Kwa heshima kubwa nawaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu waipokee, waipitie, wajadili na hatimae waipitishie bajeti ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

**161. Mheshimiwa Spika,** kwa kumalizia hotuba yangu hii, naomba kutumia fursa hii adhimu kuwashukuru Wananchi wa Jimbo letu la Chwaka kwa kuniunga mkono kwao na kwa kunivumilia katika kipindi chote cha kutekeleza majukumu yangu ya Uwaziri. Naahidi kwamba nitaendelea kuwatumikia kwa uadilifu na kushirikiana nao katika kuliendeleza Jimbo la Chwaka.

**162. Mheshimiwa Spika,** naliomba Baraza lako Tukufu liipokee, lijadili na kutushauri na hatimae liipitishae Bajeti hii.

**163. Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja.

**(Mheshimiwa Issa Haji Ussi Gavu)**

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti  
wa Baraza la Mapinduzi  
Zanzibar.

**Kiambatisho Nam. 1: Mapitio ya Upatikanaji wa Fedha kwa Kazi za Kawaida 2018/2019**

JINA LA IDARA	PROGRAMU NDOGO	BAJETI KWA MWAKA WA 2018/2019	FEDHA ZILIZOOMBWA KWA MIEZI TISA	FEDHA ZA MIEZI TISA 2018/2019	ASILIMIA YA FEDHA KWA MIEZI TISA	ASILIMIA YA FEDHA KWA MWAKA	ASILIMIA YA FEDHA KWA MIEZI TISA
Ofisi ya Faragha ya Rais	Kusimamia Huduma na Shughuli za Mheshimiwa Rais	4,557,865,000	4,408,576,885	4,408,576,885	97	100	100
Idara ya Mawasiliano - Ikulu	Kuimarisha Mawasiliano baina ya Serikali na Wananchi	440,859,000	259,498,485	259,498,485	59	100	100
	<b>Jumla</b>	<b>4,998,724,000</b>	<b>4,668,075,370</b>	<b>4,668,075,370</b>	<b>93</b>	<b>100</b>	<b>100</b>
Ofisi ya Baraza la Mapinduzi	Programu Ndogo 1: Uratibu wa Shughuli za BLM na	404,813,000	302,501,000	302,501,000	75	100	100

JINA LA IDARA	PROGRAMU NDOGO	BAJETI KWA MWAKA WA 2018/2019	FEDHA ZILIZOOMBWA KWA MIEZI TISA	FEDHA ZA MIEZI TISA 2018/2019	ASILIMIA YA FEDHA KWA MIEZI TISA	ASILIMIA YA FEDHA KWA MIEZI TISA
	Majukumu ya KBLM/KMK					
	Programu Ndogo 2: Ufuatiliaji na Tathmini ya Utendaji kazi wa Taasisi za Umma	104,988,000	44,757,500	44,757,500	43	100
	Programu Ndogo: Utumishi na Uendeshaji wa Ofisi ya Baraza La Mapinduzi.	1,451,800,000	1,388,880,120	1,041,430,120	72	75
	<b>Jumla</b>	<b>1,961,601,000</b>	<b>1,736,138,620</b>	<b>1,388,688,620</b>	<b>71</b>	<b>80</b>

JINA LA IDARA	PROGRAMU NDOGO	BAJETI KWA MWAKA WA 2018/2019	FEDHA ZILIZOOMBWA KWA MIEZI TISA	FEDHA ZA MIEZI TISA 2018/2019	ASILIMIA YA FEDHA KWA MIEZI MWAKA	ASILIMIA YA FEDHA KWA MIEZI TISA
Idara ya Ushirikiano wa Kimataifa na Uratibu wa Wazanzibari Wanaoishi Nje	Kuratibu shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar Kikanda na Kimataifa	359,950,000	200,375,580	192,272,500	53	96
	Kuratibu shughuli za Wazanzibari wanaoishi Nje ya Nchi	178,015,000	178,015,000	178,015,000	100	100
		<b>537,965,000</b>	<b>378,390,580</b>	<b>370,287,500</b>	<b>69</b>	<b>98</b>
Idara ya Uendeshaji na Utumishi	Uratibu na Usimamizi wa Shughuli za Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa	1,507,007,000	1,236,010,945	883,025,035	59	71

<b>JINA LA IDARA</b>	<b>PROGRAMU NDOGO</b>	<b>BAJETI KWA MWAKA WA 2018/2019</b>	<b>FEDHA ZILIZOOMBWA KWA MIEZI TISA</b>	<b>FEDHA ZA MIEZI TISA 2018/2019</b>	<b>ASILIMIA YA FEDHA KWA MIEZI TISA</b>	<b>ASILIMIA YA FEDHA KWA MWAKA</b>	<b>ASILIMIA YA FEDHA KWA MIEZI TISA</b>
	Baraza la Mapinduzi						
Idara ya Mipango, Sera na Utafiti	Uratibu wa Shughuli za Mipango, Sera na Utafiti za ORMBLM	407,828,000	311,862,300	284,616,600	70	91	
Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi - Pemba	Kuratibu na kusimamia shughuli za ORMBLM - Pemba	853,994,000	652,844,615	599,817,495	70	92	
Ofisi ya Usalama wa	Usimamizi wa Usalama wa	166,582,000	135,734,500	130,595,000	78	96	



JINA LA IDARA	PROGRAMU NDOGO	BAJETI KWA MWAKA WA 2018/2019	FEDHA ZILIZOOMBWA KWA MIEZI TISA	FEDHA ZA MIEZI TISA 2018/2019	ASILIMIA YA FEDHA KWA MIEZI TISA	ASILIMIA YA FEDHA KWA MIEZI TISA
Serikali (G.S.O)	Watumishi wa Umma					
		<b>2,935,411,000</b>	<b>2,336,452,360</b>	<b>1,898,054,130</b>	<b>65</b>	<b>81</b>
	<b>Jumla</b>	<b>10,433,701,000</b>	<b>9,119,056,930</b>	<b>8,325,105,620</b>	<b>80</b>	<b>91</b>

## Kiambatisho Nam. 2: Orodha ya Shehia zilizooneshwa Sinema

NAM.	KIJUJI KILIONESHWA SINEMA	SHEHIA
1.	Makoongwe	Shehia ya Makoongwe
2.	Ndooni	Shehia ya Kisiwa Panza
3.	Kimeleani	Shehia ya Fundo
4.	Michamvi	Shehia ya Michamvi
5.	Pagali	Shehia ya Pagali
6.	Bwejuu	Shehia ya Bwejuu
7.	Jendele	Shehia ya Jendele
8.	Ntebe	Shehia ya Mahonda
9.	Bumbwini	Shehia ya Kiongwe
10.	Chaani	Shehia ya Bandamani
11.	Kibuteni	Shehia ya Kibuteni
12.	Jumbi	Shehia ya Jumbi
13.	Kisauni	Shehia ya Kisauni
14.	Kidagoni	Shehia ya Kidoti
15.	Mlilile	Matemwe Kaskazini

**Kiambatisho Nam. 3: Orodha ya Vipindi Viliyoyorushwa Hewani na Idara ya Mawasiliano na Habari  
Ikulu – Zanzibar Kupitia Kituo cha ZBC Radio (A)**

<b>NAM.</b>	<b>JINA LA KIPINDI</b>	<b>TAREHE YA KURUSHWA HEWANI</b>
1.	Utekelezaji wa ahadi za Dk Shein - Kisiwa cha Uvinje.	4/7/2018
2.	Maoni ya wananchi juu ya Uimarishaji wa soko la samaki na mboga, Tibirinzi pamoja na maoni juu ya Msimu Mpya wa Uchumaji wa zao la Karafuu.	18/7/2018
3.	Maoni ya Wanadiaspora kuelekea katika Kongamano la Tano la Diaspora Tanzania.	1/8/2018
4.	Kongamano la Tano la Diaspora 2018.	22/8/2018
5.	Uimarishaji wa sekta ya utalii - UWEMAJO.	5/9/2018
6.	Uimarishaji wa sekta ya utalii - PAJE.	19/9/2018
7.	Maendeleo ya kijiji cha Mgonjoni (Sehemu ya 2).	3/10/2018
8.	Maoni ya wananchi wa kijiji cha Vitongoji - Maendeleo ya miundombinu ya barabara.	17/10/2018
9.	Utekelezaji wa Ahadi ya Uimarishaji wa Kitengo cha Kinywa na Meno - Hospitali ya Kivunge.	21/11/2018
10.	Maoni ya wananchi juu ya Sherehe za Miaka 55 ya Mapinduzi ya Zanzibar. Kisiwani, Pemba.	26/12/2018

<b>NAM.</b>	<b>JINA LA KIPINDI</b>	<b>TAREHE YA KURUSHWA HEWANI</b>
11.	Ziara ya Dk Shein Wilaya ya Mjini - Uwekaji wa Mawe ya Msingi Matangi ya Maji - Tangi la Mnara wa Mbao na Tangi la Maji la Saateni.	6/3/2019
12.	Ziara ya Dk Shein - Uwekaji wa jwe la Msingi Skuli ya Kwarara Msingi.	27/2/2019
13.	Ziara ya Dk Shein kisiwa cha Uzi.	6/3/2019
14.	Ufunguzi wa Madarasa manne Skuli ya Sekondari Kijini Matemwe.	13/3/2019
15.	Uwekaji wa jwe la msingi kituo cha Afya cha Magirisi.	20/3/2019
16.	Ziara ya Dk Shein Wilaya ya Micheweni - Kutembelea mashimo ya mchanga na Uzinduzi wa madarasa manne ya Skuli ya Sekondari Mchanga Mdogo.	27/3/2019
17.	Ziara ya Dk Shein - Ufunguzi wa kituo cha Afya cha Ngomeni.	Kipo katika hatua ya uhariri

### Vipindi Viliyovrushwa na Radio Jamii

<b>NAM.</b>	<b>MAUDHUI YA KIPINDI</b>	<b>REDIO HUSIKA</b>
1.	Afya na malezi ya mtoto	Redio Mtegani FM
2.	Haki ya elimu jamii (Pat 1 - 3)	Redio Mtegani FM
3.	Ajira kwa vijana	Redio Mtegani FM
4.	Uzaliishaji	Redio Mtegani FM
5.	Malaria	Redio Mtegani FM
6.	Mazingira yetu (Part 1 - 5)	Redio Mtegani FM
7.	Ukataji wa miti mibichi	Redio Tumbatu FM
8.	Muako wa jamii	Redio Tumbatu FM

### Vipindi vya Televisheni ZBC (B)

<b>NAM.</b>	<b>JINA LA KIPINDI</b>	<b>TAREHE YA KURUSHWA HEWANI</b>
1.	Utekelezaji wa ahadi za Dk Shein - Kisiwa cha Uvinje	5/7/2018
2.	Kongamano la 5 la Diaspora 2018	16/8/2018
3.	Utekelezaji wa Ahadi ya Uimarishaji wa Kitendo cha Kinywa na Meno - Hospitali ya Kivunge	21/11/2018
4.	Mazoezi ya Viungo – Chake Chake, Pemba	1/1/2019
5.	Ufunguzi wa Msingi Chimba	1/2/2019

<b>NAM.</b>	<b>JINA LA KIPINDI</b>	<b>TAREHE YA KURUSHWA HEWANI</b>
6.	Uzinduzi wa vituo vya uokozi na uzamiaji vya KMKM Mkoani, Pemba	2/1/2019
7.	Uzinduzi wa uwanja wa Mao Zedong	3/1/2019
8.	Uzinduzi wa Barabara ya Fuoni Mambosasa	5/1/2019
9.	Uwekaji wa Jiwe la Msingi ZURA House - Kikwajuni	6/1/2019
10.	Mfunguzi wa Maabara ya Mkemia Mkuu	8/1/2019
11.	Ufunguzi wa Skuli ya Bwefum	9/1/2019
12.	Utoaji wa Nishani	9/1/2019
13.	Kilele cha Sherehe za Miaka 55 ya Mapinduzi ya Zanzibar	12/1/2019
14.	Sherehe za taarab ya Maadhimisho ya Miaka 55 ya Mapinduzi ya Zanzibar	12/2/2019
15.	Maadhimisho ya Siku ya Sheria - Wete	4/2/2019
16.	Kuhutubia Bunge la Afrika Mashariki – BLW, Chukwani	26/2/2019
17.	Kuapishwa kwa Viongozi Walioteuliwa	4/3/2019
18.	Siku ya Wanawake Duniani - Mama Mwanamwema Shein	8/3/2019
19.	Kuapishwa kwa Viongozi Walioteuliwa	13/3/2019

<b>NAM.</b>	<b>JINA LA KIPINDI</b>	<b>TAREHE YA KURUSHWA HEWANI</b>
20.	Semina elekezi kuhusu matumizi ya ardhi na rasilimali zizorejesheka	16/3/2019
21.	Ziara ya Dk. Shein Wilaya ya Mjini - Uwekaji wa Mawe ya Msingi Matangi ya Maji - Tangi la Mnara wa Mbao na Tangi la Maji la Saateni	20/3/2019
22.	Ufunguzi wa Skuli ya Pangawe	23/3/2019
23.	Ziara ya Dk Shein kisiwa cha Uzi	27/3/2019

**Kiambatisho Nam. 4: Idadi ya Wafanyakazi Waliopatiwa Mafunzo**

**Mafunzo ya Muda Mrefu**

NAM.	OFISI NA IDARA	STASHAHADA		SHAHADA YA KWANZA		SHAHADA YA UZAMILI		SHAHADA YA UZAMIVU		JUMLA	FANI
		Me	Mke	Me	Mke	Me	Mke	Me	Mke		
1.	Ofisi ya Faragha ya Mheshimiwa Rais		1			1		1	1	3	Sheria, Maktaba na Ukairimu
2.	Idara ya Uendeshaji na Utumishi		2		1	1				4	Utunzaji Kumbukumbu, Ukatibu Muhtasi, Rasilimali Watu na Sheria
3.	Idara ya Mawasiliano na Habari - Ikulu				1					1	Mawasiliano
4.	Idara ya Mipango, Sera na Utafiti				1					1	Takwimu



NAM.	OFISI NA IDARA	STASHAH ADA		SHAHADA YA KWANZA		SHAHADA YA UZAMILI		SHAHADA YA UZAMIVU		JUMLA	FANI
		Me	Mke	Me	Mke	Me	Mke	Me	Mke		
5.	Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza - PEMBA		1	1						2	Uhasibu na Rasilimali Watu
6.	Ofisi ya Baraza la Mapnduzi		2	1	2					5	Manunuzi, Utawala, Uongozi, Uhifadhi wa nyaraka, Kumbukumbu, Sera na Utafiti.
7.	Idara ya Ushirikiano wa Kimataifa na Uratibu wa Wazanzibari Wanaoishi Nje ya nchi					2	1			3	Ushirikiano wa Kimataifa na Diplomasia ya Uchumi
	<b>Jumla Ndogo</b>	<b>0</b>	<b>3</b>	<b>5</b>	<b>6</b>	<b>1</b>	<b>1</b>	<b>1</b>	<b>1</b>	<b>20</b>	

### Mafunzo ya Muda Mfupi

NAM.	IDARA	ME	MKE	JUMLA	FANI
1.	Ofisi ya Faragha ya Rais	8	10	18	Usimamizi wa Utalii na Ukarimu.
2.	Idara ya Uendeshaji na Utumishi	114	83	197	Ukarimu, Utunzaji Kumbukumbu, Ukatibu Muhtasi, Udereva, Sheria mpya ya Manunuzi, Itifaki, Kujiandaa na Kustaafu, Kuhifadhi Kumbukumbu za Kifedha na Maradhi yasioambukiza.
3.	Idara ya Mipango, Sera na Utafiti	4	0	4	Fani ya Bajeti, Fani ya Ufuatiliaji na Tathmini, Fani Uandaaji na Usimamizi wa Miradi na Fani ya Sera za Utumishi wa Umma.
4.	Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza - PEMBA	3	2	5	Mafunzo ya Kompyuta.
5.	Ofisi ya Baraza la Mapinduzi	19	11	30	Itifaki, Ukarimu, Maandalizi ya Ajira Ufuatiliaji na Tathmini, Diplomasia ya Uchumi na Elimu ya Afya.
	<b>Jumla Ndogo</b>	<b>148</b>	<b>106</b>	<b>254</b>	
	<b>Jumla Kuu</b>	<b>158</b>	<b>116</b>	<b>274</b>	

**Kiambatisho Nam. 5: Idadi ya Watumishi Waliokwenda likizo**

<b>NAM.</b>	<b>JINA LA OFISI NA IDARA</b>	<b>ME</b>	<b>MKE</b>	<b>JUMLA KUU</b>
1.	IDARA YA MAWASILIANO NA HABARI - IKULU	3	0	<b>3</b>
2.	IDARA YA MIPANGO, SERA NA UTAFITI	1	0	<b>1</b>
3.	IDARA YA UENDESHAJI NA UTUMISHI	8	6	<b>14</b>
4.	IDARA YA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA NA URATIBU WA WAZANZIBARI WANAOSHINIJE YA NCHI	2	0	<b>2</b>
5.	OFISI YA RAIS NA MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI - PEMBA	5	6	<b>11</b>
6.	OFISI YA BARAZA LA MAPINDUZI	11	5	<b>16</b>
7.	OFISI YA FARAGHA YA RAIS	26	19	<b>45</b>
	<b>Jumla Kuu</b>	<b>56</b>	<b>36</b>	<b>92</b>

**Kiambatisho Nam. 6: Idadi ya Wafanyakazi waliofanyiwa upekuzi na Taasisi walizotoka**

NAM.	WIZARA/TAASISI	IDADI
1.	Baraza la Wawakilishi	20
2.	Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ)	14
3.	Chuo cha Uandishi wa Habari	12
4.	Chuo cha Utawala wa Umma (IPA)	05
5.	Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA)	30
6.	Idara ya Serikali Mtandao (E – Government)	19
7.	Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU)	09
8.	Kamisheni ya Utalii	16
9.	Mahakama Kuu Zanzibar	63
10.	Mamlaka ya Mafunzo ya Amali Zanzibar	24

NAM.	WIZARA/TAASISI	IDADI
11. M	Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar (ZAA)	27
12.	Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF)	11
13.	Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais	79
14.	Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG)	02
15.	Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP)	01
16.	Ofisi ya Msajili wa Hakimiliki Zanzibar	11
17.	Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali	27
18.	Ofisi ya Mufti	02
19.	Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora.	21
20.	Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi	20
21.	Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum	62

NAM.	WIZARA/TAASISI	IDADI
22.	Shirika la Bandari	192
23.	Shirika la Bima la Zanzibar (ZIC)	05
24.	Shirika la Huduma za Maktaba	02
25.	Shirika la Magazeti Zanzibar	11
26.	Shirika la Nyumba la Zanzibar (ZHC)	14
27.	Shirika la Umeme (ZECO)	05
28.	Shirika la Viwango Zanzibar (ZBS)	15
29.	Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia	07
30.	Taasisi ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi Zanzibar (ZAECA)	44
31.	Taasisi ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati (ZURA)	11
32.	Tume ya Kurekebisha Sheria	09
33.	Tume ya Kurekebisha Tabia na Dawa za Kulevya	02

NAM.	WIZARA/TAASISI	IDADI
34.	Tume ya Mipango	35
35.	Tume ya Utangazaji	02
36.	Wakala wa Kusimamia Viwanda vidogo vidogo (SMIDA)	06
37.	Wakala wa Serikali wa Uchapaji (ZAGPA)	116
38.	Wizara ya Afya	390
39.	Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira	31
40.	Wizara ya Biashara na Viwanda	40
41.	Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali	448
42.	Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto	53
43.	Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi	102
44.	Wizara ya Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo	88
	<b>Jumla</b>	<b>2,113</b>

## **Kiambatisho Nam. 7: Orodha ya Taasisi Zilizofanyiwa Ukaguzi wa Kiusalama**

1. Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ) Unguja, Dar Es Salaam na Mtwara,
2. Makaazi ya Makamo wa Pili wa Rais yaliyopo Dodoma na Dar Es Salaam,
3. Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais wa Zanzibar - Pemba na Taasisi/Idara zilizo chini yake,
4. Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kusini Pemba,
5. Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi – Unguja, Dar Es Salaam na Dodoma,
6. Ofisi ya Uratibu Shughuli za SMZ Dar Es Salaam, na
7. Ofisi ya Wakala wa Majengo ya Serikali.



**Kiambatisho Nam. 8: Idadi ya Watumishi Waliopewa Mafunzo ya Udhhibiti wa Siri na Utunzaji wa Nyaraka za Serikali**

NAM.	WIZARA/TAASISI	IDADI
1.	Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Uguja na Pemba.	141
2.	Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Uguja.	87
3.	Benki ya Watu wa Zanzibar Uguja, Pemba, Mtwara na Dar Es Salaam.	291
4.	Ofisi ya Makamu wa Piji wa Rais wa Zanzibar Dodoma, Dar Es Salaam, Uguja na Pemba (Pamoja na Idara na Vitengo vilivyopo chini yake).	118
5.	Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Uguja.	34
	<b>Jumla</b>	<b>671</b>

## **Kiambatisho Nam. 9: Orodha ya Nyaraka za Sera na Sheria Zilizojadiliwa na Baraza la Mapinduzi**

1. Mapendekezo ya kufuta Sheria ya Vyama vya Ushirika Nambari 4 ya mwaka 1986 na kutunga Sheria mpya ya Vyama vya Ushirika,
2. Mapendekezo ya kufutwa Sheria ya kukuza vitega Uchumi nambari 11/2004 na kutunga Sheria mpya badala yake,
3. Mapendekezo ya Mswada wa Sheria ya Msaada wa Kisheria,
4. Mapitio ya Sera ya Nishati ya mwaka 2009,
5. Marekebisho ya Sheria Namba 1 ya mwaka 2006 ya Mazishi ya Viongozi wa Kitaifa ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,
6. Marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Siasa, Sura 258 ya mwaka 1992,
7. Mswada wa Sheria na Marekebisho ya Sheria mbali mbali ya mwaka 2018,
8. Mswada wa Sheria ya kuanzishwa Wakala wa kusimamia Miundombinu ya Mkongwe wa Taifa Zanzibar,
9. Rasimu ya Mapendekezo ya Marekebisho ya Sheria Namba 4 ya mwaka 2010 ya Mamlaka ya Hifadhi na Uendeshaji wa mji Mkongwe Zanzibar,
10. Rasimu ya Sera ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi Zanzibar,
11. Rasimu ya Sera ya Ulinzi wa Taifa,

12. Rasisimu ya Sheria ya kuanzishwa kwa Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo,
13. Sera ya Huduma Ndogo Ndogo za Kifedha (Microfinance Policy),
14. Sera ya Maendeleo ya Viwanda Zanzibar,
15. Sera ya Maendeleo ya Viwanda, Mkakati pamoja na Tathmini.
16. Sera ya Utoaji na Matumizi ya Visiwa Vidogo Vidogo,
17. Sera ya Viwanda na Mpango wa Utekelezaji wake, na
18. Sheria ya kuanzisha Makao Makuu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dodoma.

**Kiambatisho Nam. 10: Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Bajeti 2019/2020**

<b>PROGRAMU KUU/PROGRAMU NDOGO</b>	<b>MSHAHARA</b>	<b>UENDESHAJI OFISI (OC)</b>	<b>MATUMIZI YA MAENDELEO</b>	<b>MAPENDEKEZO 2019/2020</b>
<b>Kusimamia shughuli za Mheshimiwa Rais na Kuimarisha Mawasiliano Ikulu</b>	<b>2,348,127,000</b>	<b>1,826,185,000</b>	-	<b>4,174,312,000</b>
Programu Ndogo ya Kuratibu shughuli na kusimamia huduma za Mheshimiwa Rais	2,204,701,000	1,519,113,000		3,723,814,000
Kuimarisha Mawasiliano baina ya Serikali na Wananchi	143,426,000	307,072,000	-	450,498,000

<b>PROGRAMU KUU/PROGRAMU NDOGO</b>	<b>MSHAHARA</b>	<b>JENDESHAJI OFISI (OC)</b>	<b>MATUMIZI YA MAENDELEO</b>	<b>MAPENDEKEZO 2019/2020</b>
<b>Usimamizi wa Mjukumu ya Kikanda na Kisheria ya Baraza la Mapinduzi</b>	-	<b>592,393,000</b>	-	<b>592,393,000</b>
Uratibu wa shughuli za Baraza la Mapinduzi na majukumu ya Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi	-	477,855,000	-	477,855,000
Ufuatiliaji na Tathmini ya utendaji kazi wa Taasisi za Umma	-	114,538,000	-	114,538,000
<b>Utumishi na Uendeshaji wa</b>	<b>974,200,000</b>	<b>565,507,000</b>	-	<b>1,539,707,000</b>

<b>PROGRAMU KUU/PROGRAMU NDOGO</b>	<b>MSHAHARA</b>	<b>JUENDESHAJI OFISI (OC)</b>	<b>MATUMIZI YA MAENDELEO</b>	<b>MAPENDEKEZO 2019/2020</b>
<b>Ofisi ya Baraza la Mapinduzi</b>				
Utumishi na uendeshaji wa Ofisi ya Baraza la Mapinduzi	974,200,000	565,507,000	-	1,539,707,000
<b>Kuratibu Ushirikiano wa Kikanda, Mashirika ya Kimataifa na Wazanzibari Wanaoishi Nje ya Nchi</b>	<b>139,528,000</b>	<b>508,795,000</b>	-	<b>648,323,000</b>
Kuratibu Shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Kikanda na Kimataifa	139,528,000	275,475,000	-	415,003,000

<b>PROGRAMU KUU/PROGRAMU NDOGO</b>	<b>MSHAHARA</b>	<b>JUENDESHAJI OFISI (OC)</b>	<b>MATUMIZI YA MAENDELEO</b>	<b>MAPENDEKEZO 2019/2020</b>
Kuratibu Shughuli za Wazanzibari Wanaoishi nje ya Nchi	-	233,320,000	-	233,320,000
<b>Utumishi na Uendeshaji wa Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi</b>	<b>1,201,244,000</b>	<b>1,570,520,000</b>	<b>2,000,000,000</b>	<b>4,771,764,000</b>
Uratibu na Usimamizi wa Shughuli za Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi	703,421,000	722,848,000	-	1,426,269,000
Uratibu wa Shughuli za Mipango, Sera na Itifiti za CRM/IRM	83,895,000	264,755,000	2,000,000,000	2,348,650,000

<b>PROGRAMU KUU/PROGRAMU NDOGO</b>	<b>MSHAHARA</b>	<b>UENDESHAJI OFISI (OC)</b>	<b>MATUMIZI YA MAENDELEO</b>	<b>MAPENDEKEZO 2019/2020</b>
Uratibu na Usimamizi wa Shughuli za ORMBLM - Pemba	413,928,000	392,407,000	-	806,335,000
Kusimamia Usalama wa Watumishi wa Umma	-	190,510,000	-	190,510,000
<b>JUMLA KUBWA</b>	<b>4,663,099,000</b>	<b>5,063,400,000</b>	<b>2,000,000,000</b>	<b>11,726,499,000</b>



**Kiambatisho Nam. 11: Orodha ya Wageni Waliofika Ikulu na Kuonana na Mheshimiwa Dk. Ali Mohamed Shein – Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Kuanzia Mwezi wa Julai, 2018 Hadi Mwezi wa Aprili, 2019**

<b>TAREHE</b>	<b>JINA LA MGENI</b>	<b>CHEO</b>
<b>JULAI, 2018</b>		
27.07.2018	Mheshimiwa Hawa Olga Ndilowe	Balozi wa Malawi nchini Tanzania
29.07.2018	Mheshimiwa Jasem Ibrahim Al-Najem	Balozi wa Kuwait nchini Tanzania
<b>AGOSTI, 2018</b>		
09.08.2018	Mheshimiwa Reem Ebrahim Al-Hashemy	Waziri wa Nchi wa Umoja wa Falme za Kiarabu (U.A.E) anayeshughulikia Ushirikiano wa Kimataifa akifuatana na ujumbe wake
17.08.2018	Mheshimiwa Job Yustino Ndugai	Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
17.08.2018	Dkt. Bashiru Ally	Katibu Mkuu wa CCM
20.08.2018	Mheshimiwa Gervais Abayeho	Balozi wa Burundi nchini Tanzania, akifuatana na:
	Mheshimiwa Pre'fe're Ndayishimiye	Naibu Balozi wa Burundi nchini Tanzania

<b>TAREHE</b>	<b>JINA LA MGENI</b>	<b>CHEO</b>
28.08.2018	Prof. Florens D.M. Luoga	Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania (BOT) akifuatana na:
	Dkt. Berbard Y. Kibesse	Naibu Gavana, Usimamizi wa Sekta ya Fedha
	Dkt. Yamungu Kayandabula	Naibu Gavana, Sera na Uchumi wa Fedha
	Bwana Julian Raphael	Naibu Gavana, Utawala na Udhhibiti wa Ndani
	Bwana Suleiman Said Masoud	Kaimu Mkurugenzi wa (BOT), Tawi la Zanzibar
<b>SEPTEMBER, 2018</b>		
10.09.2018	Dkt. Maimbo William Mindolwa	Askofu Mkuu wa Kanisa la Anglikana Tanzania akifuatana na:
	Askofu Michael Henry Hafidh	Askofu wa Dayosisi ya Zanzibar
17.09.2018	Mheshimiwa Dan Kazungu	Balozi wa Jamhuri ya Kenya nchini Tanzania
	Jaji Francis S. K. Mutungi	Msjili wa Vyama vya Siasa nchini Tanzania akifuatana na:
25.09.2018	Bwana Mohamed Ali Ahmed	Naibu Msajili wa Vyama vya Siasa
	Bwana Athumani Diwani Msuya	Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU)
<b>OKTOBA, 2018</b>		
04.10.2018	Mheshimiwa Job Yustino Ndugai	Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akifuatana na:

<b>TAREHE</b>	<b>JINA LA MGENI</b>	<b>CHEO</b>
	Mheshimiwa Edde Mukabagwiza	Naibu Spika wa Bunge la Rwanda
	Mheshimiwa Stephen Kagaigai	Katibu wa Bunge na Katibu wa Kanda ya Afrika wa CPA
	Bwana Said Yakubu	Katibu wa Spika
	Bwana Demetrina Mgalama	Katibu Msaidizi wa CPA Kanda ya Afrika
12.10.2018	Mheshimiwa Aziz Ponary Mlima	Balozi wa Tanzania nchini Uganda
18.10.2018	Mheshimiwa Dk. Hassan Diab	Waziri wa zamani wa Elimu ya Juu nchini Lebanoni na Makamu wa Rais wa American University of Beirut – Lebanon
23.10.2018	Mheshimiwa Sheikh Saud bin Saqr Al-Qasimi	Mtawala wa Ras-Al- Khaimah
	Dorothy Temu Usiri	Mratibu wa Umoja wa Mataifa (UN), Ofisi ya Zanzibar akifuatana na:
25. 10.2018	Bwana Helge Flard	Mshauri Mkuu Ofisi ya Mratibu wa Umoja wa Mataifa
	Bibi Rukiya Wadoud	Mkuu wa Ofisi ndogo ya Umoja wa Mataifa, Zanzibar

<b>TAREHE</b>	<b>JINA LA MGENI</b>	<b>CHEO</b>
<b>NOVEMBA, 2018</b>		
06.11.2018	Dkt. Abdalla Juma Saadal Mabodi	Naibu Katibu Mkuu wa CCM, Zanzibar
16.11.2018	Mheshimiwa Hamid M.H. Abuali	Balozi wa Palestine nchini Tanzania
	Dkt. Evindh Hamsen	Afisa Mtendaji Mkuu wa Hospitali ya Chuo Kikuu cha Haukeland nchini Norway, akifuatana na:
16.11.2018	Dkt. Dohn Wigum Dahil	Mkurugenzi
	Prof. Stenner Kvinnsland	Mshauri Mkuu
	Dkt. Trond Mohn	"Philanthropist"
18.11.2018	Mheshimiwa Cai Defeng	Makamu Mwenyekiti wa Baraza Kuu (Congress) la Jamhuri ya Watu wa China
	Mheshimiwa Kangji Lugola (Mb)	Waziri wa Mambo ya Ndani wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, akifuatana na:
19.11.2018	Major Gen. Jacob G. Kingu	Katibu Mkuu
	Bwana Ramadhan K. Kailima	Naibu Katibu Mkuu
	Bwana Fred Kafeero	Mwakilishi Mkaazi wa Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO), akifuatana na:
30.11.2018	Dr. Jacob Oduor	Benki ya Maendelo ya Afrika
	Bibi Jenny Correia Nunes	Umoja wa Nchi za Ulaya

<b>TAREHE</b>	<b>JINA LA MGENI</b>	<b>CHEO</b>
	Bwana Stephen Bainous. Kargbo	Mwakilishi Mkaazi wa Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Maendeleo ya Viwanda (UNIDO) nchini Tanzania, Mauritius na Afrika Mashariki
	Bwana Fumiliko Suzuki	Afisa wa Shirika la Sirika la Maendeleo la Kimataifa Japani, Tanzania
	Dr. Mwatima Abdalla Juma	Mkuu wa programu ya "IFAD", Tanzania
	Bwana Juvenal Kisanga	Afisa Mkuu wa programu ya Shirika la Chakula Duniani" nchini Tanzania
	Bwana Vianey Rweyendela	Meneja wa "AGRA Tanzania"
	Bwana Emmanuel Kihaule	Afisa Habari wa Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa
<b>DISEMBA, 2018</b>		
03.12.2018	Sheikh Ali Rashid Lootah	Mwenyekiti wa Kampuni ya AI - Nakheelya Dubai
04.12.2018	Bibi Maniza Zaman	Mwakilishi Mkaazi wa Shirika la Mfuko wa Umoja wa Mataifa unaoshughulikia Maendeleo ya Watoto (UNICEF), akifuatana na:
	Bibi Maha Damai	Afisa Mkuu wa "UNICEF", Ofisi ya Zanzibar

<b>TAREHE</b>	<b>JINA LA MGENI</b>	<b>CHEO</b>
04.12.2018	Dkt. Tigest Ketsela Mangestu Bwana Ghirmony Andomichael Dkt. Ahmed Eltigani Abdwel Rahim Elmansouri Bwana Saddam Ahmed Ally	Mwakilishi Mkaazi wa Shirika la Afya Duniani (WHO) nchini Tanzania, akifuatana na: Afisa Mkuu wa "WHO", Ofisi ya Zanzibar Kampuni ya Al-Rawabi inayomiliki Kiwanda cha maziwa jijini Sharjah, akifuatana na: Afisa Uhusiano kutoka Ubalozi wa Umoja wa Nchi za Falme za Kiarabu (UAE) nchini Tanzania Balozi wa Jamhuri ya Korea nchini Tanzania, akifuatana na: Afisa kutoka Ubalozi wa Korea Naibu Mhasibu Mkuu wa Benki ya Exim ya Korea, Ofisi ya Dar Es Salaam
04.12.2018	Mheshimiwa Song Geum – Young Bwana Jiin AN Bwana Hyeonjeng Choir	Mheshimiwa Song Geum – Young Bwana Jiin AN Bwana Hyeonjeng Choir
06.12.2018	Mheshimiwa Abdalla Sultan Alowais	Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wafanyabiashara na Wenyewe Viwanda kutoka Sharjah, ambaye pia ni Mwenyekiti wa Kampuni ya Al-Rawab akifuatana na: Makamu Mwenyekiti
07.12.2018	Mheshimiwa Sheikh Majid bin Faisal Al-qassimi	Makamu Mwenyekiti

<b>TAREHE</b>	<b>JINA LA MGENI</b>	<b>CHEO</b>
10.12.2018	Mheshimiwa Mohammed Al-Suwaidi	Mjumbe wa Bodi ya Jumuiya
	Mheshimiwa Nasser Al-Tunajji	Mjumbe wa Bodi ya Jumuiya
	Bwana Abdelaziz Shattaf	Afisa Mtendaji Mkuu wa Jumuiya
	Bwana Ahmed Al-Mansouri	Afisa Mtendaji Mkuu wa Jumuiya
	Bwana Saddam Ahmed Ally	Afisa Uhusiano wa Ubalizi wa UAE, Dar Es Salaam
	Mheshimiwa Gaudentia Kabaka (MNEC)	Mwenyekiti wa Umoja wa Wanawake (UWT) - Taifa, akifuatana na:
	Mheshimiwa Thuwayba E. Kissasi	Makamu Mwenyekiti - UWT
	Bibi Queen Mlozi	Katibu Mkuu – UWT
	Bibi Tunu J. Kondo	Kaimu Naibu Katibu Mkuu – UWT
	Bibi Catherine Peter Nao	Mjumbe Kamati Tekelezaji - UWT
	Bibi Mwaka Abraham	Mjumbe Kamati Tekelezaji - UWT
	Mheshimiwa Mwanaidi Kassim (MBLW)	Mjumbe Kamati Tekelezaji - UWT
Ndugu Lucy Edward Mwakyeembe	Mjumbe Kamati Tekelezaji - UWT	

<b>TAREHE</b>	<b>JINA LA MGENI</b>	<b>CHEO</b>
<b>JANUARI, 2019</b>		
28.01.2019	Mheshimiwa Mubarak Faleh Mohammed Al Sehajjan	Balozi wa Kuwait nchini Tanzania
28.01.2019	Mheshimiwa Yonas SanbeYosef	Balozi wa Ethiopia nchini Tanzania
28.01.2019	Mheshimiwa Gaber Mohammed Abulwafa	Balozi wa Jamhuri ya Kiarabu ya Watu wa Misri nchini Tanzania
<b>FEBRUARI, 2019</b>		
03.02.2019	Mheshimiwa Dkt. Ezzaldin Omar	Waziri wa Kilimo na Masuala ya Ardhi wa Jamhuri ya Kiarabu ya Watu wa Misri
15.02.2019	Prof. Biang Yuhong	Mhadhiri kutoka Chuo cha Tiba Mchanganyiko Tianjin nchini China, akifutana na:
	Dkt. Siambi Kikete	Daktari kutoka nchini Kenya
<b>MACHI, 2019</b>		
01.03.2019	Mheshimiwa Dkt. Damas Daniel Ndumbaro (Mb)	Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki
04.03.2019	Mheshimiwa Jaji Fransic S. K. Mutungi	Msjajiwa wa Vyama vya Siasa nchini Tanzania, akifuatana na:
	Bwana Mohamed Ali Ahmed	Naibu Msajili wa Vyama vya Siasa, Zanzibar



<b>TAREHE</b>	<b>JINA LA MGENI</b>	<b>CHEO</b>
08.03.2019	Bwana Liehui	Mwenyekiti wa Kampuni ya "Touchroad Group" ya China
12.03.2019	Mheshimiwa Jaji Mstaafu Hamid Mahmud	Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi, Zanzibar
19.03.2019	Bwana Olivier Adam	Mratibu Mkuu wa Taasisi ya Wafanyakazi wa Kujitolea wa Umoja wa Mataifa akifuatana na:
	Bwana Njoya Tikum	Meneja wa Kanda ya Mashirika ya Kusini mwa Afrika kutoka Jumuiya ya kujitolea wa Umoja wa Mataifa
	Bwana Caristian Mwamanga	Mkuu wa wafanyakazi wa Kujitolea wa Umoja wa Mataifa kwa Tanzania
	Bwana Edga Kiliba	Mchambuzi mitandao ya Mawasiliano katika Ofisi ya ratibu Mkaazi wa Umoja wa Mataifa
	Bibi Rukiya Wadoud	Mtaalamu wa uendeshaji wa utekelezaji wa Programu ya Ofisi ndogo ya UNDP, Zanzibar
22.03.2019	Bibi Dorothy Temu Usiri	Mratibu wa Umoja wa Mataifa wa shughuli za eneo la Zanzibar
	Mheshimiwa Hassan Simba Yahya	Balozi wa Tanzania nchini Zambia

<b>TAREHE</b>	<b>JINA LA MGENI</b>	<b>CHEO</b>
<b>APRILI, 2019</b>		
11.04.2019	Bibi Dame Louise Martin	Rais wa Shirikisho la Michezo ya Jumuiya ya Madola, akifuatana na:
	Bibi Miriam Moyo	Makamu wa Rais, Kanda ya Afrika
	Bwana Gulam A. Rashid	Rais wa Kamati ya Olimpiki, Tanzania (TOC)
	Bwana Henry Benny Tandau	Makamu wa Rais (TOC)
	Bwana Filbert Bayi	Katibu Mkuu (TOC)
11.04.2019	Mheshimiwa Prof. Palamagamba Kabudi (Mb)	Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki